




## SPIKA aongoza mazishi ya mwakilishi aliyeanguka kwenye baraza

UKURASA 2




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Machi 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581239

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## CCM yaonya wateule wa Rais kero za wananchi kuibuliwa na wakubwa

UKURASA 2



Nehemiah Mchechu

# Mahakama yaamuru Mchechu kulipwa fidia bilioni 2.5/-

UKURASA 4



Meneja Masoko wa Benki ya KCB Tanzania, Shose Kombe (wa tatu kushoto), akizungumza na baadhi ya wateja waliofika katika maonyesho ya wanawake na vijana wajasiriamali yaliyoandaliwa na taasisi ya TAWEN, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto miaka 16 adaiwa kujinyonga kisa 8,000/-

UKURASA 8


SPECIAL SUPPLEMENT

**WOMEN'S DAY** 8th March

The Guardian Nipashe



The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the **Women's Day** theme

**Embrace Equity**

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Advetorials** and **Advertisements.**

**TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701**

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com


**MICHEZO** SIMBA: TUMEANDAA MPANGO KAZI MPYA UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Joseph Ntakirutimana (wa nne kushoto), aliyeambatana na ujumbe wake, Ikulu ndogo ya Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# CCM yaonya wateule wa Rais kero kuibuliwa na wakubwa

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amewataka wateule wa Rais kushuka chini zaidi kwa wananchi ili kusikiliza na kutatua kero zao badala ya kusubiri ziibuliwe kwenye ziara za viongozi wakubwa.

Amesema viongozi hao wanapaswa kuhangaika na matatizo ya wananchi na watambue kuwa hata mawasiliano ya simu ni kwa ajili ya kupokea kero za Watanzania, hivyo wanapaswa kutoa namba zao za simu ili wananchi wawapigie.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa shina namba mbili la Kijiji cha Mtinko wilayani Singida, Chongolo alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewafungia kuwasuka upya wateule wake ili watakapotoka huko, waongeze kasi kwenye utendaji kazi zao na kwenda kwa wananchi kujua na kutatua kero zao.

"Rais amewafungia mahali anawasuka upya ili wakitoka huko waje na kasi zaidi, ameniambia anajua leo (jana) nimeingia Halmashauri ya Singida Vijijini kitu ambacho hakiendi sawa nimweleze ili kusukuma zaidi.

"Ninajua hapa mna hospitali yenu ya wilaya lakini haijaletewa fedha za kutosha, hivyo anasema ataleta fedha nyingi zaidi," alisema.

Alisisitiza CCM haiendi kwa wananchi kupiga maneno, bali kujua kero na kuzitatua na kuangalia maeneo ambayo hayaendi vizuri ili kuongeza kasi.

"Mimi ninachokifanya ni kuja kwa wananchi kusikiliza kero kwa kuwa ninyi ndio mmetupa dhamana ya kuongoza, haipendezi kiongozi mkubwa unakwenda mahali unakutana na malalamiko ambayo viongozi waliopo huko wana jukumu la kutatua.

"Niwahimize wakuu wa mikoa na wilaya hakikisheni mnashuka chini zaidi kwa wananchi kusikiliza kero na kuwatatulia, niwapongeze Mkoa wa Singida kila mahali ninapokwenda wanasema tumelipeleka kwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya," alisema.

Juzi akijibu hoja mbalimbali za wananchi katika mkutano na wananchi wa Nduguti wilayani Mkalama, Chongolo alisema viongozi wanapotatua hoja za wananchi, wanatekeleza majukumu yao na huo ndio uongozi na si kuwa watukufu.

Alimpongeza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alipopigiwa simu na mwananchi kuhusu mahitaji ya mbolea, alichukua hatua na kuagiza ipelekwe na ilifika eneo hilo ili kuwasaidia wakulima.

"Waziri, Mkuu wa Mkoa, Wilaya, Katibu Tawala, Tarafa na wengine wote, sio watukufu, ni watumishi, lazima wawajibike na wajue kwamba wamepewa dhamana kwa ajili ya Watanzania," alisema. Awali Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema alisema uongozi ni kuongoza kwa vitendo na kuwataka viongozi wa CCM kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu kwenda kwa wananchi kusikiliza kero na kuzitatua.

"Kazi anayofanya Rais ni kazi kwa vitendo. Kwa miaka miwili amefanya yale yote yanayotakiwa, kila mmoja atimize wajibu wake kwenye eneo lake, kupanga ni kuchagua utapumzika ukimaliza kazi zako," alisema.

Katibu wa NEC Idara ya Organaizesheni, Issa Gavu aliwakumbusha viongozi kuhakikisha wanachama wanalipa ada ili kuwa na haki ya kuchagua na kuchaguliwa. Aliwahimiza viongozi wa shina kukaa vikao na wanachama ili kujua kero zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi na kusimamia kwa kauli moja watakayokubaliana.

"Katibu Mkuu amekuja kuangalia utekelezaji wa ilani, sisi CCM serikali yetu inatekeleza yale yaliyoagizwa na tumeahidi mengi tukiamini uwezo wa viongozi wetu na ahadi zote tutazikamilisha na mwaka 2025 sisi tutashinda tena kutokana na tulichoahidi kimetekelezwa," alisema.

***Augusta Njoji na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

# Wanaume watajwa kikwazo huduma kwa wajawazito

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MRATIBU wa Afya ya Uzazi na Mtoto kwenye Kituo cha Afya Mlandizi, Kibaha, Happiness Ndelwa amesema kitendo cha baadhi ya wanaume kushindwa kushiriki kwenda kliniki na wake zao ni sehemu ya vikwazo katika ununuzi wa vifaa vinavyotakiwa wakati wa kujifungua.

Ndelwa amesema baadhi ya wanawake wanafika kwenye kituo hicho bila kuwa na vifaa wanavyotakiwa kuwa navyo wakati wa kujifungua, jambo ambalo linaufanya uongozi wa hospitali kufanya jitihada kuvipata.

Alibainisha hayo jana wakati Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo alipotembelea kituo hicho na wodi za wazazi kujionea mazingira ya kujifungulia na vikwazo vilivyoko kwenye kituo hicho.

"Wapo baadhi ya wanaume hawataki kushiriki na wake zao kuja hospitalini, wanaona kufanya hivyo ni kupoteza muda bila kujua kuwa huko ndiko wanaelezwa kila kitu anachotakiwa mama mjamzito kubeba anapokuja kujifungua," alisema Ndelwa.

Mratibu huyo alimwomba mbunge huyo wanapokuwa kwenye mikutano yao, kuzungumzia suala hilo ili kuwaondolea vikwazo wauguzi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Yahaya Mbogolume alimweleza mbunge huyo kuwa wapo wanawake wanaofika kujifungulia kituoni bila vifaa walivyoelekezwa mbali na vinavyotolewa na serikali.

Awali Muuguzi Kiongozi Wodi ya Wazazi kwenye kituo hicho, Exaveria Kapulula alisema kuna wakati wazazi wanalazimika kulala kitanda kimoja wawili baada ya kujifungua kutokana na ongezeko la wateja kwenye wodi hiyo.

Kapulula alisema uwezo wa kituo hicho kwenye wodi ya wazazi ni kuhudumia wanawake 77 kwa mwezi, lakini wanaofika kujifungua wamekuwa wakifikia 282 kwa muda tajwa.

Mwakamo alisema serikali inafahamu vikwazo kwenye huduma za afya na zinaendelea kutatuliwa ili wananchi wanufaike na kuondokana na msongamano uliopo kwenye baadhi ya vituo.

# Spika aongoza mazishi mwakilishi aliyeanguka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid ameongoza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuuaga mwili wa Mwakilishi wa Mtambwe Pemba, Habib Ali Mohamed aliyefariki dunia juzi kwenye Hospitali ya Saifee mkoani Dar es Salaam.

Habib alianguka ghafla kwenye jengo la Baraza la Wawakilishi wakati anajiandaa kuingia kushiriki kikao cha asubuhi na kukimbizwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na baadaye kusafirishwa kwenda Dar es Salaam kwenye Hospitali ya Saifee.

Spika Zuberi alisema uongozi wa Baraza la Wawakilishi umesikitishwa na msiba huo mkubwa ambao ni pigo kwa taifa, familia pamoja na wananchi wa Jimbo la Mtambwe pamoja na Chama cha ACT-Wazalendo alichokuwa akikiwakilisha.

Alisema Mohamed atakumbukwa kutokana na mchango wake mkubwa wakati akiwa mwakilishi wa jimbo hilo kutokana na michango yake iliyojikita katika kuwatetea wananchi na taifa lake.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla alisema mwakilishi huyo atakumbukwa kutokana na uwezo wake wa kuwawakilisha wananchi wa jimbo lake kwa uaminifu wa hali ya juu.

"Pengo lake ni kubwa, na kwa niaba ya Serikali ya Zanzibar, inawasilisha salamu za pole kwa ndugu na jamaa pamoja na chama cha ACT-Wazalendo kwa msiba mkubwa," alisema.

Mohamed alizaliwa Mtambwe Juni 22, 1960 na kusoma Shule ya Msingi Uondwe, Pemba mwaka 1967 na sekondari katika Shule ya Ufundi ya Karume iliyoko Unguja aliyosoma mwaka 1973 hadi 1976.

Mwaka 1979-1982 alisoma elimu ya juu huko Urusi kwenye chuo cha ufundim akichukua kozi za masuala ya viwanda na aliporejea nchini, aliajiriwa kwenye Kiwanda cha Makonyo, Pemba.

Alipanda cheo hadi kufikia mkurugenzi katika kiwanda hicho anayeshughulikia masuala ya uzalishaji.

Kwa upande wa chama, amekuwa kiongozi katika ngazi mbalimbali ikiwamo kuanzia wadi ya Jimbo la Mtambwe hadi mwaka 2020 alipochukua fomu kuwania jimbo hilo na kuibuka na ushindi.

## HABARI KITAIFA




Sehemu ya wazee wa Mkoa wa Dodoma, walioandamana huku wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali wa kudai haki zao, kuanzia eneo la Majengo na kuishia viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bilionea Mmarekani kupata malighafi kutoka Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI maombi yake ya leseni ya kutoa huduma za intaneti kupitia kampuni yake ya Starlink yakiwa yamewekewa kigingi na masharti ya serikali, Bilionea Mmarekani Elon Musk amepenya kwenye soko la Tanzania ambapo atanunua malighafi ya kutengenezea betri za magari ya umeme.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari wiki hii na wawakilishi wa kampuni hiyo, inasema kwamba kampuni ya Musk ya Tesla inayotengeneza magari ya umeme, imeingia mkataba wa kununua hadi tani 35,000 za malighafi aina ya Anode Active Material inayotumika kutengenezea betri za magari ya umeme kwa mwaka kutoka kampuni ya Magnis Energy Technologies Limited ya Australia kupitia kampuni yake tanzu ya Kitanzania ya Uranex Tanzania Limited.

"Tesla imekubali kununua kati ya tani 17,500 na 35,000 za Anode Active Material kwa mwaka kutoka Magnis Energy Technologies kuanzia mwezi Februari 2025 kwa kipindi cha miaka mitatu," inasema taarifa hiyo.

Tofauti na kuingiza fedha za kigeni, taarifa hiyo imesema makubaliano hayo yamekuja wakati mwafaka kwa sababu Tanzania kama nchi inategemea kunufaika zaidi na ajira pamoja na ujuzi kwa watu wake.

Uranex Tanzania Limited inamilikiwa na Magnis Energy Technologies Limited ya Australia na mradi wake wa uchimbaji wa madini ya kinywe (graphite) wa Nachu Graphite Project ulioko Ruangwa mkoani Lindi unajulikana duniani kwa kutoa bidhaa bora za madini hayo.

Tesla yenye makao yake jijini Austin, Marekani ni kampuni inayoongoza kwa utengenezaji wa magari ya umeme ambayo yanapigiwa chapuo na wanaharakati wa mazingira kama usafiri rafiki kwa mazingira kulinganisha na magari yanayotumia bidhaa za petroli yanayolaumiwa kwa kutoa hewa ukaa na kuongeza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Katika makubaliano hayo, Uranex Tanzania itasimamia mradi wa kinywe wa Nachu kuhakikisha inatoa bidhaa bora kwa ajili ya kusafirishwa kwenda kwa mteja ambaye ni Tesla.

Tangu mwaka jana, taarifa zilisambaa kwamba Bilionea Musk ambaye ni Mmarekani aliyezaliwa Afrika Kusini, aliwasilisha maombi nchini kupitia kampuni yake ya Starlink ya kuomba leseni ya kutoa huduma nafuu ya intaneti kupitia satelaiti.

Na hivi karibuni kulikuwa na sintofahamu kuhusu hatma ya maombi yake huku kukiwa na fununu kwenye mitandao ya kijamii kwamba aliwekewa mizengwe na kampuni za simu zinazotoa huduma za intaneti kwa Watanzania wengi kwa sasa.

Lakini Jumanne wiki hii, Nape Nnauye, Waziri wa Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, alilitolea ufafanuzi suala hilo, akisisitiza kwamba hakuna mizengwe bali kuna masharti ambayo mwomba leseni hajatekeleza.

"Kuna mambo mawili; kwanza tuliwaambia wafungue ofisi hapa Tanzania ili kukiwa na matatizo ya kimtandao, wateja wao waende hapo na si ofisini kwangu. Pili, tuliwaomba watuthibitishie namna watakavyotunza taarifa za wateja wao," alisema waziri huyo wakati wa ziara yake kwa vyombo vya habari vya IPP mkoani Dar es Salaam mwanzoni mwa wiki.

# Walioguswa mradi wa bomba la mafuta wakabidhiwa nyumba

**Na Mwandishi Wetu,**
MULEBA

ILIKUWA furaha na tabasamu kwa wanakijiji 10 wa Nkomelo wilayani Muleba mkoani Kagera baada ya kukabidhiwa nyumba zao mpya kama sehemu ya fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unaotarajiwa kuanza kujengwa baadaye mwaka huu.

Nyumba hizo walizokabidhiwa wanakijiji hao zina huduma zote muhimu, ikiwa ni pamoja na jiko na vyoo vya nje, mifumo ya nishati ya jua, matangi kwa ajili ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita 5,000 kwa kila nyumba na vitu vingine muhimu yakiwamo madirisha ya kisasa ya vioo.

"Kusema kweli sikuwahi kufikiria kumiliki nyumba nzuri kama hii maishani mwangu kwa sababu nilikuwa ninaishi kwenye nyumba ndogo ya udongo, lakini kumiliki nyumba ya kisasa ni jambo ambalo sikuwahi kufikiria hapo awali," alisema Jovin Bebwa Thadeo, mwenye umri wa miaka 67, baba wa watoto 15.

Dustan Muganyizi (54) wakati akipokea ufunguo wa nyumba ya familia yake, alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa na furaha na hakuweza kuizuia isionekana wazi.

"Pia tulipokea fedha za fidia ambazo zilibadilisha maisha yetu kabisa kwa kutuwezesha kufanya vitu mbalimbali vya kimaendeleo kama vile kununua pikipiki, mashamba ya ziada na mifugo (ng'ombe)," alisema.

Muganyizi, baba wa familia ya watoto watano, aliongeza kuwa kupewa nyumba ni sehemu ya fidia ambayo imeboresha maisha yao.

Wawakilishi waandamizi kutoka EACOP, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na viongozi wa serikali wilayani Muleba walihudhuria hafla hiyo ya kukabidhi nyumba hizo.

Mkurugenzi wa Biashara ya Petroli wa TPDC, Dk. Wellington Hudson alisema jumla ya nyumba 292 zitajengwa kwa ajili ya watu waliopisha mradi ambapo kati ya hizo, 58 tayari zimejengwa kwenye maeneo mbalimbali litakalopita bomba hilo.

Alisema makabidhiano hayo ya nyumba kwa waliguswa na mradi ni ishara tosha kwamba mchakato wa fidia kwa waliguswa na mradi unaendelea bila vikwazo vyovyote.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa EACOP, Martin Tiffen, kabla ya kutia saini mikataba, wananchi waliguswa na mradi walishirikishwa katika mchakato wa malipo na tathmini kwa ajili ya fidia zao.

Alisema kuwa watu 9,898 waliguswa na mradi ambapo asilimia 97 sehemu yao ya mashamba ndio imepitiwa na mradi.

Alisema watu 344 ambao ni sawa na asilimia tatu iliyobaki, nyumba zao ndizo zimepitiwa na mradi na zitabomolewa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa bomba hilo la mafuta ghafi.

Bosi huyo wa EACOP aliongeza kuwa asilimia 90 ya watu hao ambao nyumba zao zinapitiwa na mradi walifanya uamuzi wa busara wa kuchagua kujengewa nyumba mbadala za zege ambazo zinajengwa na makandarasi wazawa kwa kutumia ubunifu kutoka Afrika Kusini.

Aliongeza kuwa nyumba hizo mbadala ziko chini uangalizi kwa mwaka mmoja ambapo makandarasi watawajibika kurekebisha uharibifu wowote utakaotokea katika kipindi hicho.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA, Prof. Mark Mwandosya alipongeza hatua ya EACOP kukabidhi nyumba hizo kwa walengwa, akisema inatoa ujumbe kwa wanaopinga mradi huo kuwa haki za binadamu pia zinazingatiwa katika utekelezaji wake.

"Tunazingatia matakwa yote ya jumuiya za kimataifa ikiwa ni pamoja na ulinzi wa mazingira na uhifadhi tunapotekeleza mradi huu wa kimkakati wa kitaifa.

"Tuliahidi katika kutekeleza mradi huu kuwa tutalinda mazingira na kuboresha maisha ya watu wetu kijamii na kiuchumi," alisema Prof. Mwandosya ambaye alishika nyadhifa tofauti za uwaziri katika serikali ya awamu ya nne.

Aziz Mlima, Balozi wa Tanzania nchini Uganda, alisema Tanzania iko katika hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huo na kusema kuwa amefurahishwa na hatua iliyofikiwa kwenye maeneo tofauti ya mradi huo aliyowahi kuyatembelea.

Ntaki Charles Mayunga, Kaimu Mtendaji wa Wilaya ya Muleba aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya, Abel Nyamahanga, alisema ujenzi wa nyumba hizo umekuwa na tija katika kukuza uchumi wa wakazi wa Nkomelo kwa kutengeneza ajira.

EACOP imepewa leseni ya kujenga miundombinu ya usafirishaji wa mafuta ghafi yenye urefu wa kilomita 1,443 ambazo zitasafirisha mafuta ghafi kutoka Kabaale - Hoima, Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika soko la kimataifa.

## TANGA FORESTS LIMITED

**The companies Act, 2002 (Section 345)**

**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **TANGA FORESTS LIMITED** a company with registration number **54988** dully intends to convene a final meeting on 4th April, 2023 in accordance to section 345(2) of the Companies Act, 2002. The purpose of the general meeting is laying before the accounts and giving any explanation thereof.

All parties concerned and who have claims are hereby called to attend the meeting at **Basil & Alred office, Ace Building (1st Floor), Haile Selassie Road, Dar es salaam, Tanzania on 4th April, 2023 at 10am.**

**GODFREY BASIL MRAMBA**
**Liquidator**
**For TANGA FORESTS LIMITED**

217308402

# Mahakama yaamuru gazeti kumlipa Mchechu bil. 2.5/-

**Na Mwandishi Wetu**



MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, imeiamuru kampuni ya Mwananchi Communications Limited (MCL) kumlipa fidia ya jumla ya Sh. bilioni 2.5 Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu.

Uamuzi huo wa mahakama umetokana na kuridhika na madai yaliyowasilishwa na Mchechu, ambaye hadi wiki iliyopita, alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwamba kampuni hiyo, kupitia gazeti lake la The Citizen, ilichapisha habari iliyomchafua na kumshushia hadhi kitaifa na kimataifa.

Mchechu aliwasilisha madai hayo mahakamani kupitia mawakili wake, Aliko Mwamenenge na Vitalis Peter, kutokana na gazeti hilo katika toleo lake la Machi 23, 2013 kuchapisha habari yenye kichwa kinachosomeka 'Why JPM dissolved NHC Board, sacked Mchechu', kwa tafsiri isiyo rasmi 'Kwa nini JPM (John Magufuli- aliyekuwa Rais) alivunja Bodi ya NHC, kumfukuza Mchechu'.

"Machi 23, 2018 ilikuwa siku ya kiza kwangu. Ni siku ambayo niliandikwa na gazeti la the Citizen ukurasa wa mbele habari ambayo ililenga kunichafua, kunishushia hadhi, kunikosanisha na jamii kubwa ya Watanzania na kuonekana kuwa mtu nisiyefaa kabisa kuwa kiongozi au sehemu ya jamii njema ya Watanzania. Mtu nisiye na maadili, nisiyeaminika na kimsingi nisiyestahili hata kuongoza popote," alidai Mchechu alipotoa ushahidi wake kesi ilipoanza kusikilizwa.

Katika uamuzi huo wa kesi ya madai Na. 48/2031 uliosomwa na Jaji Leila Mgonya aliyekuwa akisikiliza shauri hilo, kampuni hiyo imeamuriwa kumlipa Mchechu Sh. bilioni mbili ikiwa ni fidia kwa kuchafuliwa na Sh. milioni 500 kutokana na kushushiwa hadhi yeye na familia yake. Mchechu aliomba mahakama iamuru alipe fidia ya Sh. bilioni tatu na gharama zingine zilizotokana na kushushiwa hadhi yake.

Sambamba na kulipa fedha hizo, kampuni ya MCL inatakiwa kulipa riba ya asilimia 12 kwa mwaka wa fedha zilizoamuriwa kumlipa mlalamikaji iwapo kutakuwa na ucheleweshaji pamoja na gharama za uendeshaji wa kesi hiyo.

Jaji Mgonya alisema katika kufikia uamuzi huo, mahakama ilijielekeza katika masuala manne yakiwamo kama habari hiyo ililenga kumkashfu mlalamikaji, athari alizozipata kutokana na taarifa hiyo, ukweli juu ya madai yaliyoibuliwa kutokana na habari yenyewe.

Alisema katika hoja ya kwanza kama habari hiyo ilikuwa na lengo la kumchafua na kuonekana si mwaminifu, kinara wa wizi, mtu asiye na uwezo na sifa za kuongoza taasisi ya umma, ushahidi alioutoa Mchechu katika kujenga kesi yake umethibitisha kuwa ulikuwa na malengo hayo.

Kwa mujibu wa Jaji, habari hiyo haikuwa na ukweli wowote kwamba Mchechu alifukuzwa na (Hayati) Rais Magufuli kama ilivyodaiwa na hata video zilizotolewa kama ushahidi hazikuthibitisha hivyo.

"Katika video zilizoonyeshwa ikiwamo ya Azam TV zilizoletwa mahakamani kama ushahidi wa upande wa utetezi, hakuna sehemu iliyoonyesha kwamba Rais Magufuli alimfukuza Mchechu," alisema Jaji Mgonya na kuongeza kuwa hata wakati habari hiyo inachapishwa, Mchechu alikuwa bado mwajiriwa wa NHC hadi Juni, 2018.

Aidha, Jaji alisema jambo lingine linaloonyesha kuwa habari hiyo haikuwa na nia njema ni kutokana na utetezi kushindwa kuwasilisha ushahidi juu ya madai yaliyoibuliwa ikiwamo taarifa kutoka ndani ya taasisi zilizodaiwa kuchunguza madai dhidi ya Mchechu ikiwamo Bodi ya Wakurugenzi wa NHC. Sababu nyingine, alisema ni kukosekana kwa ushahidi kuhusu vikao vya bodi ya NHC kufanyika Dubai.

"Walipaswa kuwasilisha ushahidi kwamba walikwenda lini Dubai na ni watu wangapi, walifikia hoteli gani na gharama zilizotumika ni kiasi gani," alisema Jaji.

Katika habari hiyo pia ilidaiwa kuwa Mchechu alikuwa akichunguzwa kutokana na mgongano wa kimaslahi kuhusu utafutaji na upatikanaji wa ekari 500 za mradi wa NHC wa Safari City jambo ambalo Mchechu alidai si kweli wakati akitoa ushahidi wake na kwamba shirika halijawahi kununua eneo la ukubwa huo.

Aidha, ilidaiwa kuwa ardhi ya mradi huo, awali iliripotiwa kununuliwa na kampuni inayomilikiwa na Mchechu ambayo ilinunua kutoka kwa raia wa kigeni na uchunguzi ulionyesha kuwa aliiuzia NHC kwa bei ya juu.

Sambamba na madai hayo, ilidaiwa kuwa Mchechu akitumia mkandarasi wa NHC kutengeneza barabara kwenda kwenye eneo lake lililo karibu na eneo la mradi wa Safari City huku gharama zikiwa zinabebwa na shirika.

Katika uamuzi wake, Jaji alisema madai hayo yote hayakuthibitishwa na upande wa utetezi kwa kushindwa kuwasilisha vielelezo kuonyesha uhalali au ukweli wa madai hayo.

Kuhusu Mchechu kumiliki ardhi katika jiji la Arusha karibu na mradi wa NHC wa Safari City, pia utetezi umeshindwa kutoa ushahidi licha ya kwamba katika video iliyowasilishwa, Magufuli alikaririwa akidai (Mchechu) ana kampuni inayofanya kazi kama za NHC lakini haikusemwa ni wapi na kampuni yenyewe haikutajwa.

"Ni kweli Magufuli alisema hayo kuwa ana viwanja na anaandika majina ya watu lakini hakutaja wapi na hata jina la kampuni yake halikutajwa," alisisitiza.

Kuhusu neno 'sack' ambalo liliibua ubishani baina ya mawakili wa mlalamikaji na walalamikiwa, Jaji Mgonya alisema lina maana ya moja kwa moja kwamba ni kufukuzwa na si vinginevyo. Upande wa utetezi ulidai kuwa neno hilo maana yake ni mtu kusimamishwa au kuondolewa katika nafasi yake na si kufukuzwa kama ilivyodaiwa na mawakili wa Mchechu.

Pia alisisitiza neno hilo lilikuwa na tafsiri ya moja kwa moja kuwa Magufuli alimfukuza Mchechu na hakuna sehemu ya hotuba yake iliyotajwa hivyo. Pia alisema hakuna 'slogan' wala staili ya kitaaluma katika uandishi kama utetezi ulivyodai.

Kuhusu madai ya kampuni ya bima ambayo mmoja wa wakurugenzi ni mke wa Mchechu kupewa zabuni ya kuziwekea bima nyumba za NHC Mtwara, pia hayajathibitishwa mbele ya mahakama na kuonekana hazina ukweli wowote.

Jaji Mgonya pia alisema habari hiyo ilikiuka misingi ya haki kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo haki ya kusikilizwa kwa kuwa Mchechu hakupewa nafasi kabla ya kuchapishwa kwake.

Kutokana na ushahidi uliojengwa, Jaji alisema mlalamikaji ametoa ushahidi na hoja katika viwango vinavyotakiwa na kuthibitisha pasina chembe ya shaka kwamba habari hiyo ilikuwa na lengo la kumchafua, kumshushia hadhi na kumvunjia heshima katika jamii.

**MADAI YA MCHECHU**

Kutokana na habari hiyo, Mchechu alidai kuwa licha ya kumshushia hadhi, habari hiyo ilisababisha akose kuaminika, hivyo kupoteza nafasi nyingi za kibiashara alizokuwa anafanya pamoja na kuondokewa na wabia katika kampuni ambazo ana uhusiano nazo kibiashara.

"Taarifa hii ilinisababishia mfadhaiko mkubwa wa akili, msongo wa mawazo hofu na kudhuru afya yangu. Pia ilinipotezea nafasi ya maendeleo yangu kikazi na kunipotezea mapato ya ajira yangu na ushiriki wangu katika bodi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Pia alidai alilazimika kujiuzulu baadhi ya nyadhifa.

Mchechu pia alidai wakati habari hiyo inaandikwa, alikuwa katika mchakato wa kupata nafasi ya ofisa mtendaji mkuu wa taasisi ya kimataifa ya kifedha katika masuala ya makazi ya Shelter Afrique, hivyo kusababisha kukosa licha ya kwamba alikuwa akiongoza katika mchakato huo.

Pia kutokana na nafasi yake ya uongozi katika kanisa, akiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Fedha ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, alikosa kuaminika na kuwapo hofu ya usalama wa sadaka za waumini.

Aliongeza kuwa: "Kwa kweli habari hii imenifanya nionekane mlafi, tapeli, mlanguzi, mtu ninayetumia vibaya nafasi yangu."

# NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER MSHANA | BUNJU-KINONDONI | 15/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | TANDALE | 14/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 28/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 14/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 15/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | NYUMBA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | USTAWI-MWANZA | 15/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA-MWANZA | 14/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MANGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA VIWILI VYENYE HATI MILIKI | MANGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 15/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | KIWANJA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | BUJINGWA-MWANZA | 14/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FIKIRI SAID MSISI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FIKIRI SAID MSISI | MBONDOLE | 21/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | CESILIA SAMWEL KWEKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA KUU | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | RAYNSONS AND COMPANY | NYUMBA | RAYMOND MICHAEL MREMI | KIBAHA | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MOHAMED ABDALLAH LUTAMBI | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI | MOHAMED ABDALLAH LUTAMBI | KIBAHA | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | NYUMBA | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | TANDALE | 24/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | FLORA JULIUS KIMUNE | NYUMBA | FLORA JULIUS KIMUNE | KIPUNGUNI | 21/03/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UKONGA | HASSANI RAMADHANI GOGO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | HASSANI RAMADHANI GOGO | TUNGINI CHANIKA-ILALA | 21/03/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | 1.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO 2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.59847 KIWANJA NA.2009 KITALU ''D'' | 1.LAMECK JOHN RUGIGA 2.CRISPIN PATRICK KAPILIMBA | 1.MBEZI MSHIKAMANO 2.SINZA | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GERALD VENANCE SALLEH | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.85778 KIWANJA NA.2166 KITALU ''B'' MBEZI LUIS | GERALD VENANCE | MBEZI LUIS | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ZARINA SAID RAJABU | NYUMBA | AKIDA ABDUL SIRAJI | TEGETA ''A'' | 21.03.2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. KND011648 | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | HAPPYNESS DANIEL RWEHUMBIZA | NYUMBA | DAUDI MUSA SUNTA | MBEZI MSUMI | 30/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ITU COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 93457 KIWANJA NAMBA '1', KITALU 'G' MAPINGA ,KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 89175 KIWANJA NA. '1157', KITALU 'A' TEGETA KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA | ANDREW ANTHONY SINDABAHA | 1.MAPINGA BAGAMOYO 2.TEGETA | 17/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | SABRINA SAIDI MAULIDI | NYUMBA | RAMADHANI SAID MUNGU | MALAMBA MAWILI | 06/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SHABANI RASHIDI NAENJE | NYUMBA | SHABANI RASHIDI NAENJE | MLAMLEMI MKURANGA | 20/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | RASHIDI HAMADI CHALAMILA | NYUMBA | RASHIDI HAMADI CHALAMILA | MLAMLEMI MKURANGA | 20/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ELLEN DANIEL RYOBA | NYUMBA | ELLEN DANIEL RYOBA | AMANI KIPUNGUNI | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ABDALLA SALUM SAID | NYUMBA | CHRISTINA CRISTIAN KAIJAGE | PUGU STESHENI | 28/04/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DEVOTA JOHN KATINDASA | NYUMBA | MASOUD HAMAD SEIF | KICHANGANI MAJOHE | 11/05/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM DARUWESHI IDDI | NYUMBA | MARIAM DARUWESHI IDDI | KIBUGUMO-KIGAMBONI | 18/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ISIMBULA MAULID RAJABU | KIWANJA | ISIMBULA MAULID RAJABU | MURIET -ARUSHA | 20/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MASANJA AJMES WANNA | KIWANJA | MASSANJA JAMES WANNA | MURIET -ARUSHA | 20/03/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JOHN LEONARD MAIGE | KIWANJA | JOHN LEONARD MAIGE | MURIET -ARUSHA | 20/03/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 21/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | ELISHA AMELYE CHENGULA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | ELISHA AMELYE CHENGULA | MLOWO -MBEYA | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BENARD ANAEL CHUNGU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | BENARD ANAEL CHUNGU | IYOTO-MBEYA | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ALEX MATHEW MWAIPYANA | NYUMBA | ALEX MATHEW MWAIPYANA | KINYEREZI | 21/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | HUSSEIN NASIBU JUMA | NYUMBA | DEVOTA FRUMENTUS MBUGA | MAILI MOJA KIBAHA | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HNP AND GENERAL SUPPLY LIMITED | NYUMBA | HELLY PETER NYONI | KIGAMBONI DEGE | 23/03/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | ANNANEEMA DANIEL RITTE | KIWANJA | ANNANEEMA DANIEL RITTE | SEGU CHINI, KATA YA NALA - DODOMA | 20/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | HAWA HATIBU MUNISI | NYUMBA | RESTUS JULIUS KIMATH | NYASAKA-MWANZA | 24/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | NYUMBA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | GEITA | 21/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SIKITU HAMIS YAHAYA | NYUMBA | HAJI ABEID KASUBI | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | LUCAS NTIRUHUNGWA MZYENGE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAPHET YONA MZAVA | KIGAMBONI | 24/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM SAIDI TUMBO | NYUMBA | DAHIMU KASSIMU CHKWAWA | YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE | 15/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | NYUMBA | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | YOMBO VITUKA-SIGARA | 15/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 14/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | NYUMBA | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | MBEZI MTONI-MTONGANI | 16/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | MNANDALA SAIDI MSAFIRI | NYUMBA | MNANDALA SAIDI MSAFIRI | PUGU | 17/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | MAGRESTH RHOBI SASI | NYUMBA | MAGRESTH RHOBI SASI | MBONDOLE MSONGOLA | 21/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | KAIMU SAID AMANZI | NYUMBA | KAIMU SAID AMANZI | MVULENI-MSONGOLA | 21/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ZULFA SHAFII MALENDA | NYUMBA | HALIMA SHAFII MALENDA | NZASA -CHARAMBE | 17/03/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | UYACODE VICOBA PROGRAM | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KNDO 29299-KND/MBR/MWZ/10/2 | UYACODE VICOBA PROGRAM HQ | MAKUBURI UBUNGO | 15/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ZAINABU RASHIDI LUKWELE | NYUMBA | OMARI SAIDI MAINGO | MKURANGA | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 23/03/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TANDALE | MARYAN GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | MARYAN KAPAMA | KIMARA | 24/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | BUMERA LOGDE AND CO LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | KIGOGO KATI | 30/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 23/03/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | FAISAL SALUM HASSAN | GARI T396 DJR HINO RAINBOW | FAISAL SALUM HASSAN | TEMEKE | 24/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | SHERAL SELEMANI HUSSEIN | GARI TATA BUS T357 DSR | SHERAL SELEMANI HUSSEIN | MBAGALA MAJIMATITU | 24/03/2023 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.***0715868000/0753575752/0765999000/0754376493/0759282344/0718038313/0655715138***
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217308602

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Nidhamu bado ni tatizo wachezaji Ligi Kuu Bara

**WAKATI** msimu wa mwaka 2022/2023 wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaelekea ukingoni, suala la nidhamu kwa wachezaji wanaoshiriki ligi hiyo ya juu nchini limeonekana kuwa ni tatizo.

Msimu huu unaelekea ukingoni pia kwa Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la Kwanza, First League (Ligi Daraja la Pili) na Ligi Kuu Zanzibar.

Kwa upande wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, ambayo inashirikisha timu 10 kutoka mikoa mbalimbali ya hapa nchini, yenyewe ndio inataka kuingia katika mzunguko wa lala salama kuanzia Jumatano ijayo.

Nidhamu imekuwa tatizo si kwa wachezaji wazawa, lakini imeonekana ni shida pia hata kwa wachezaji wa kigeni ambao wanacheza hapa nchini.

Mara kadhaa wachezaji ambao walikuwa nyota na tegemeo katika vikosi vya timu zao, wameonekana kufanya vitendo vya utovu wa nidhamu na kwa namna moja au nyingine, uamuzi huo huchangia kuiumiza timu.

Lakini bila kusahau, mchezaji anayesimamishwa au kufukuzwa kwa kosa la kinidhamu, si tu anakipunguzia nguvu kikosi cha timu yake, basi ajue anakiweka kipaji chake katika mazingira tata kuelekea msimu mpya ambao timu huhitaji kusajili nyota wenye uwezo na ubora mkubwa. Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wachezaji kuweka mbele nidhamu endapo wanahitaji kufanikiwa, lakini kama wanasindikiza wenzao au hapo walipo wanaona wamekamilisha ndoto zao, ni vyema wakaondoka kwa kufuata taratibu na kutoa nafasi kwa waliobakia kucheza.

Ili kumaliza tatizo hili, umefika wakati Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na timu, zikaweka kanuni na adhabu kali kwa sababu wakiendelea kuacha vitendo hivi, itachangia kuwaharibu wachezaji wetu chipukizi ambao wanatakiwa kukuza vipaji vyao kwa kuangalia kaka au dada zao wanafanya nini.

Ifike wakati mchezaji ambaye amekuwa akifanya makosa yanayojirudia mara kwa mara au kutoitumikia klabu yake ipasavyo kama ilivyotarajiwa, akatakiwa kulipa faini, hii itasaidia kuongeza nidhamu na kila mchezaji kutekeleza majukumu yake vyema.

Kwa mfano utasikia mchezaji, mara kadhaa inaelezwa ana matatizo ya kifamilia, akifanya mazoezi kwa wakati anaotaka, lakini huyo huyo anaonekana akiendelea na shughuli zake binafsi, hii haijengi na haileti picha nzuri kwa nyota chipukizi walioko katika kikosi kimoja.

Kama klabu inavyoajiri au kuandaa programu maalumu za kukiongezea nguvu kikosi, ni vyema pia ikawaandalia wachezaji wake walimu watakaowasaidia kuwaandaa kufahamu hakuna kiongozi, mchezaji au mfanyabiashara ambaye alipata mafanikio kwa kuwa na nidhamu mbovu.

Hili linawezekana kuchangia kutoonekana kwa aliyekuwa mshambuliaji nyota na muhimu kwa timu katika msimu mpya, kwa sababu tu alishindwa kuwa na nidhamu hasa baada ya kupata mafanikio na kujisahau.


Ni vigumu kwa mchezaji ambaye ameitumikia timu na kupewa misingi yake, kusikika akitoa maneno yasiyo na afya pale anapotaka kuondoka au anapoona tayari ameshakuwa maarufu, mchezaji aliyekuzwa katika misingi ya nidhamu, kamwe hataweza kutoa lugha za kebehi kule alikotoka.

Kwa misingi hiyo, mchezaji mwenye nidhamu, pia hatakuwa tayari kuona wakala, meneja au mzazi wake anakuwa sehemu ya mgogoro pale linapotokea suala la kudai maslahi bora.

TFF na klabu zote tuhakikishe tunawaandaa vyema wachezaji wetu hawa wanaoshiriki ligi za hapa nchini, kwa sababu ndio tegemeo kubwa la kupata nyota wanaozitumikia timu zetu za Taifa.

Inajulikana wazi, timu bora ya Taifa ni ile inayoundwa na wachezaji wenye vipaji, wenye kujituma, wenye kujitambua, lakini wakiongozwa na nidhamu ya ndani na nje ya uwanja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Chipukizi wapewe nafasi kwenye timu za Ligi Kuu

**JUZI** kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, mshambuliaji, Mohamed Mussa, aliweka rekodi ambayo ataikumbuka kwenye maisha yake yote ya soka.

Nayo ni kufunga bao la kwanza kwa timu yake ya Simba, ambayo alijiunga nayo akitokea Malindi FC ya Zanzibar.

Straika huyo chipukizi hata atakapokuwa staa mkubwa kwenye timu hiyo, au nyingine pamoja na timu ya taifa ya Tanzania, bado atakumbuka bao hilo alilolifunga kwa sababu limemfungulia njia.

Ni ndoto ya kila mchezaji wa Tanzania, si kuzichezea klabu za Simba na Yanga tu, lakini kufunga bao.

Kwanza kabisa usajili wake si kitu ambacho kilitegemewa sana, badala yake ulifanyika baada ya Simba kwenda kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi, huku Malindi nayo ikishiriki michuano hiyo.

Taarifa kutoka Zanzibar zilisema Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' alipotua kwa mara ya kwanza kuiangalia timu hiyo mara baada ya kukabidhiwa jukumu la kuinoa, bado alikuwa anakaa jukwaani, akiitizama timu yake mpya na mechi zingine kwa ujumla.

Alimwona kijana huyo akifanya kazi akiwa na kikosi cha Malindi, akifunga mabao mawili kwenye mechi tofauti, lakini pia akahabarishwa ndiye aliyekuwa anaongoza kwa upachikaji mabao kwenye Ligi Kuu Zanzibar.

Akaomba kama kuna uwezekano asajiliwe. Hapo ndipo viongozi wa Simba walipomsajili mchezaji huyo.

Tangu juzi amekuwa gumzo kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa jinsi alivyofunga bao hilo.

Ukiliangalia hata baadhi ya mastraika ambao ni wazoefu hawawezi kufunga. Na ukitaka kuangalia hiyo tazama alipoanza kuuchukua mpira.

Kabla ya kupachika bao hilo, mpira ulianza kwa kipa, Beno Kakolanya, aliyemwanzia, Peter Banda, ambaye aliukokota na kumpasia mfungaji naye aliukokota kwa hatua kadhaa, aliupeleka kwa Moses Phiri, huku akiuomba tena awekewe mbele kwa ishara ya mikono iliyoonekana wazi.

Phiri hakufanya ajizi, aliuweka kwenye njia, huku akiwa amebanwa na mabeki wawili, Mussa aliwazidi ujanja na mbio, akaachia shuti la mguu wa kushoto mpira ukajaa wavuni kulia kwa kipa, Rajab Hamisi.

Mwingine angetoa pasi, halafu angemwacha Phiri afanye anavyotaka kufanya na angeanza kutembea.

Inaonekana kabisa ni straika mwenye uchu wa kufunga mabao, kwani alikaribia kufunga mara mbili baada ya bao hilo.

Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa wakilalamika timu yao ina wachezaji wengi ambao umri wao umekwenda sana, hivyo wanahitaji timu mpya yenye wachezaji wengi vijana.

Kama hili litafanyika basi mmoja wa wachezaji ambao wanaweza kuwika zaidi msimu ujao ni Mussa. Na kuhusu suala la kujitunza, huwa sina matatizo na wachezaji wanaotoka Zanzibar. Ndiyo maana kama ukichunguza wanacheza soka muda mrefu zaidi kuliko wa Bara.

Sisemi kama wachezaji wakongwe hawatakiwi kwenye soka au Ligi Kuu, ila timu zinatakiwa kuwapa zaidi kipaumbele wachezaji vijana ili wapate uzoefu.

Unashangaa kuona timu ina wachezaji robo tatu wana umri mkubwa, hivyo kukosa kasi na pumzi. Timu inatakiwa iwe na angalau robo ya wakongwe na robo tatu ni vijana. Na hilo ndilo Robertinho amekuwa akilitaka na kulikosa ndani ya Simba.

Tukiangalia timu nyingi za Tanzania Bara na hata Championship zinakuwa na wachezaji wale wale ambao wanacheza miaka nenda rudi. Wanazunguka tu mwaka huu akicheza timu hii, msimu ujao anacheza timu nyingine. Hii inafanya kusiwe na maingizo mapya ya wachezaji wapya wazawa kwenye Ligi Kuu.

Tunajua kwa sasa timu nyingi zinasajili wachezaji wengi kutoka nje ya nchi, lakini tunatakiwa kama nchi kuwe na ingizo kubwa la wachezaji vijana karibuni kila msimu.

Hii haitozisaidia timu za Ligi Kuu tu, lakini pia hata Taifa Stars.

Ili timu iwe bora inatakiwa iwe na wachezaji wakongwe wazoefu, lakini si wengi zaidi ya vijana, na kukiwa na wakongwe wengi kikosi kinadumaa, na vijana wakikosa nafasi.

**MAKALA**

# Usalama kazini ulivyoubeba mgodi kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

UKITEMBELEA Mgodi wa Geita Gold Mining Limited (GGML) uliopo mkoani Geita, hutoshangazwa na ushindi ambao mgodi huo umeupata kwa mara ya nne mfululizo kwenye kundi la tuzo ya kimataifa ya usalama mahala pa kazi (Global Safety Award).

Katika tuzo hiyo inayotolewa na kundi la Kampuni za AngloGold Ashanti (AGA), GGML imeshinda mwaka 2019, 2020, 2021 na wiki hii imeshinda tuzo hiyo kwa mwaka 2022.

Hii ina maana kuwa AGA ambayo inamiliki migodi kwenye nchi za Australia, Colombia, Argentina, Brazil, Ghana na Tanzania, GGML kwa ujumla ndio kinara wa kuzingatia masuala ya usalama mahala pa kazi.

Hili ni jambo ambalo hata nchi hizo zilizoendelea kuliko Tanzania, zinajiuliza imekuwaje nchi kama Tanzania iliyopo kwenye kundi la nchi zinazoendelea, inashinda tuzo hii na kuifanya GGML kuwa kampuni ya kwanza kushinda mara nne mfululizo katika historia ya nchi na AGA kwa ujumla?

Mafanikio hayo hayakuja kirahisi kama anavyoeleza Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa GGML, Dk. Kiva Mvungi kwamba ni jitihada za wafanyakazi, makandarasi na uongozi wa kampuni hiyo.



Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa GGML, Dk. Kiva Mvungi (wa pili kulia) pamoja na watendaji wa idara ya afya na usalama kutoka Geita Gold Mining Limited, wakifurahia ushindi wa nne mfululizo katika Tuzo ya Kimataifa ya Usalama Mahala pa Kazi. Kampuni hiyo imeiongoza Tanzania imezipiku nchi za Australia, Ghana na Afrika Kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### SIRI YA TUZO

Dk. Mvungi anasema siri ya mafanikio ya GGML kushinda tuzo hiyo ambayo ni zawadi ya juu kabisa, ni ushirikiano wa wafanyakazi na makandarasi ambao wamekuwa wakiuonyesha katika kujali afya zao pamoja na kujali usalama kazini.

Anasema kitu ambacho wamefanya tofauti na wenzao ni kubadilisha mfumo wa mawasiliano ya kiusalama, badala ya kutoka kwa viongozi kwenda kwa wafanyakazi, waliweka utaratibu kwamba mfumo huo wa mawasiliano utoke kwa wafanyakazi kuja kwa viongozi.

"Kwa hiyo, tunapofanya kazi, wafanyakazi na makandarasi hutuambia jambo lipi ni salama au sio salama au wangetaka lifanyike vipi, kwa hiyo sisi huongeza tu masuala mengine ya kiuongozi kuhakikisha kazi inafanyika kwa usalama," anasema.

Anafafanua kuwa tangu wameanza kutumia mfumo huo wa kuwasikiliza zaidi wafanyakazi na makandarasi, mafanikio yamekuwa makubwa katika utendaji kazi.

Anatolea mfano kuwa zaidi ya miaka 10 iliyopita hakuna mfanyakazi aliyepoteza maisha akiwa kazini, lakini pia kwa zaidi ya miaka mitano hakuna mfanyakazi aliyeumia kiasi cha kushindwa kufika kazini. GGML pia imekaa zaidi ya miaka minne bila ya kuwa na mfanyakazi aliyeumia akitekeleza majukumu yake.

Anasema GGML huwa inao mgawanyo wa kupima kiwango cha kuumia. Wafanyakazi wengi walioumia katika kipindi chote ni wale waliohitaji tu huduma ya kwanza ambapo walitibiwa na kurudi kazini.

"Mchango wetu huu umehusisha kila mtu kuanzia wale wafanyakazi wanaotekeleza majukumu ya kawaida na wafanyakazi wetu ambao wameajiriwa kwa mikataba ya muda mfupi kutoka vijiji na mitaa inayotuzunguka.

"Wote hawa tunashirikiana nao katika kuiishi tunu yetu muhimu inayosisitiza usalama ndicho kipaumbele cha kwanza katika shughuli zetu zote muhimu mgodini.

"Kwa kawaida pia tunao wawakilishi kila idara na kwa kila mkandarasi ambao hutusaidia kusimamia ubora wa afya, usalama na mazingira.

"Wawakilishi hawa ni kama wabunge, yaani wawakilishi wa wafanyakazi kwani kila wanachokiona hakipo sawa, hutoa taarifa ambayo sisi huifanyia kazi na kufanya maboresho ya usalama kwenye maeneo yetu," anasema.

Anaongeza kuwa pamoja na kwamba kimataifa GGML imetambulika, kuonekana na kushinda tuzo hiyo, nchini pia imetambuliwa na Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa kazi (OSHA), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na taasisi nyingine za afya zimekuwa zikiwapatia pongezi na tuzo mbalimbali kuonyesha wao ni bora katika masuala ya afya, usalama na mazingira pamoja na mafunzo pia.

Anasema serikali imekuwa ikiwasimamia, ikiwakagua na imewapatia maelekezo kila mara. Mathalani, wiki iliyopita OSHA walikuwa mgodini huko, kiongozi huyo akisisitiza inaonesha kiasi gani serikali inasimamia ubora wa afya na usalama mahala pa kazi kwenye mgodi huo.

Pia OSHA walipima afya za wafanyakazi pamoja na kwamba GGML pia ina madaktari wanaopima wafanyakazi wao.

"Nimpongeze kila mfanyakazi na mkandarasi aliyeshiriki kuhakikisha anapofika kazini anatekeleza majukumu yake kwa usalama na anarudi kuelekea nyumbani akiwa salama, na sisi kwenye tunu zetu, tunu namba moja ni afya na usalama ambayo ndio kipaumbele chetu, yaani kazi yoyote isifanyike kama hakuna usalama, hivyo yote mawili yanaendana kwa pamoja," anasema.

### MISINGI YA USALAMA

Dk. Mvungi anasema kampuni ya GGML imeweka misingi thabiti ya uzalishaji kwenye usalama lakini kampuni nyingine zimeweka msisitizo kwenye kupunguza gharama.

Anasema kitendo cha GGML kuwekeza kwenye usalama kina maana kuwa watu wanapofanya kazi kwa usalama, gharama za uzalishaji zinapungua na uzalishaji wenyewe unaongezeka.

Anatolea mfano kuwa ukiwa haufanyi kazi kwa usalama, magari yataharibika, mashine zitaharibika na watu wataumia na kwamba masuala yote hayo yanaweza kusimamisha mwendelezo wa uzalishaji.

"Lakini vifaa pia vikiharibika huwezi kuvitumia. Kwa mfano, una mashine moja ikiharibika kwa sababu haikutumika kwa usalama maana yake kesho haitafanya kazi, pia ukiwa na mfanyakazi akaumia, utahitaji pia kumtibu na hapo utapoteza muda na gharama, kwa kifupi unaona uhusiano kati ya usalama na uzalishaji vinaenda sambamba," anasema.

Anabainisha kuwa kwa miaka zaidi ya 10, kampuni imetimiza malengo ya mwaka inayojiwekea kwenye uzalishaji.

Anasema malengo haya wameyafikia kwa sababu ya kuimarisha usalama, akisisitiza hata nyumba ukiishi kwa usalama hakuna majanga ya moto na ajali nyingine, kipato cha familia kitaongezeka.

"Nyumbani kwetu tunapoishi, barabara tunazopita, safari tunazofanya nje, mikoani na kwingine kote tunaangalia usalama.

"Tunataka mtu alale vizuri, aangalie chombo chake cha usafiri kama ni gari akague injini, ndipo aanze safari akiwa salama na akifika katikati ya safari yake kila baada ya saa mbili aegeshe gari pembeni aangalie usalama wake, na vyote tunafuatilia. Mfano maeneo ya Geita - Mwanza ambako ni karibu na mgodi, tunafuatilia.

"Kuhusu matumizi ya vilevi, tuna utaratibu wa kupima pombe kwa wafanyakazi na tumeruhusu kama mfanyakazi alikuwa na sherehe, basi aombe ruhusa kutokuja kazini siku inayofuata, bure kabisa na mshahara wake anaendelea kulipwa ili keshokutwa aje kazini ukiwa salama," anasema.

### TATHMINI VIHATARISHI

Dk. Mvungi pia anasema katika siku za karibuni, GGML imefanya tathmini ya vihatarishi vikubwa ambavyo vipo kwenye kampuni hiyo kwa sababu wanaamini vihatarishi vikubwa wakivishughulikia au wakiviimarisha watapunguza hatari iliyopo kwenye maeneo, hivyo kuendelea kuwa salama.

Anasema mwanzo walikuwa na maeneo 18 lakini siku za karibuni, wamefanya utafiti na kupitia vihatarishi hivyo kisha kubaki na maeneo 10.

"Mfano ni vifaa vya moto na mashine zinazotembea, kufanya kazi maeneo ya juu zaidi ya mita mbili, sehemu nyingine kama vilipuzi. Kuna kemikali mbalimbali hatari tunazotumia, hayo ni maeneo ambayo tukiyafanyia kazi na kudhibiti vihatarishi tunabaki salama.

"Udhibiti huo umewekwa kwenye maeneo ya msingi kabisa na kila mfanyakazi anapofika kazini kwake, anazingatia hayo maeneo. Usalama unahusika kwa kila mtu kwenye maisha, hivyo akiangalia hivyo, anabaki salama," anasema.

### MKURUGENZI ASIFU

Akizungumzia ushindi huo wa tuzo nne mfululizo, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong ameipongeza timu nzima ya idara ya afya, usalama na mazingira pamoja na wafanyakazi wote wa GGML kwa kudumisha usalama wao ndani na nje ya kampuni.

Mbali na tuzo hiyo ya kimataifa ya usalama, anasema GGML pia ilipata tuzo ya utendaji bora kwa jumla.

"Hayo ni matokeo mazuri yanayoashiria namna tulivyofanya vyema katika usalama na utendaji kazi kwa ujumla. Ninajua ni kazi gani kubwa imefanywa katika kufanikisha hili na ninapenda kuipongeza timu ya idara ya usalama na afya ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wote, makandarasi na wasimamizi ambao wamefanya kazi kwa bidii mwaka mzima kuhakikisha kila mtu anarudi nyumbani salama kufikia malengo yetu.

"Hakika tuzo hii inaonyesha namna mmefanya vizuri na kuthaminiwa. Juhudi zenu zinatambuliwa vyema na na kampuni nzima. Kama tunavyojua sote bado tuna changamoto nyingi za kufanyia kazi kama timu na nina uhakika tunaweza kufanya kazi pamoja na kutimiza yote. Wacha tuendelee! Hongereni sana," anapongeza mkurugenzi huyo.

Mmoja wa wafanyakazi wa idara hiyo ya usalama, afya na mazingira ndani ya GGML, Dk. Subira Joseph ambaye amefanya kazi ndani ya kampuni hiyo kwa zaidi ya miaka 10 kama daktari kwenye Kituo cha Afya cha GGML pamoja na Josephine Kimambo ambaye ni mhandisi wa mazingira, wanasema ushindi mfululizo wa tuzo hiyo umewafanya waone wanafanya kazi kwenye mazingira salama.

"Kwani yasingekuwa salama hata hiyo tuzo tusingeipata. Lakini pia imenifanya nione idara yetu ya usalama, afya na mazingira kazini inafanya kazi vizuri na watu.

"Ushirikishwaji wa watu upo vizuri, watu wanaripoti vihatarishi, kwa sababu ili janga lisilete hatari lazima litolewe taarifa haraka, lisipotolewa taarifa kwa wakati hatari yake itakuwa kubwa, hivyo watu wapo makini na usalama na mazingira. Tuzo hii imenifanya nijisikie vizuri na kujivunia kufanya kazi kwenye idara hii," anasema Josephine.

Josephine naye anaungwa mkono na Mrakibu wa Usalama katika idara ya uchimbaji chini ya ardhi, Melxedeck Mulokozi ambaye amefanya kazi ndani ya GGML kwa zaidi ya miaka 14.

Anasema kushinda tuzo ya kimataifa ya usalama mahala pa kazi miongoni mwa migodi yote ya AGA kumempa faraja kubwa kwa sababu imeonyesha kwamba tangu waanze kushinda haikuwa kwa kubahatisha.

# Raia Malawi wahukumiwa kisutu

**Na Grace Gurisha**

RAIA watatu wa Malawi wamehukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kulipa faini ya Sh. milioni 1.5 na wakishindwa kila mmoja atatumikia kifungo cha mwezi mmoja gerezani.

Raia hao ni Willium Chitemji, John Phiri na Winston Kainda ambao mahakama hiyo iliwatia hatiani kwa kosa la kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemalira baada ya washtakiwa kukumbushwa makosa yao na kisha kukiri.

Hakimu Rugemalira alisema washtakiwa wote katika kosa la kuingia nchini bila kibali, anawahukumu kulipa faini Sh. 500,000 au kwenda jela mwezi mmoja.

Katika shtaka la pili ambalo ni kuishi nchini bila kibali, Hakimu Rugemalira aliwaachia washtakiwa hao kwa masharti ya kutofanya kosa hilo ndani ya mwaka mmoja.

Pia alisema wakimaliza adhabu hiyo wanatakiwa kurudishwa nchini kwao ili wafuate taratibu za kuishi nchini.

Hakimu Rugemalira alisema kuwa baada ya kusikiliza utetezi wao na namna walivyoingia nchini, aliwapunguzia adhabu ya kosa moja kwa kuwa wameshakaa mahabusu mwezi mmoja.

Kabla ya kutolewa kwa adhabu hiyo, Wakili kutoka Jeshi la Uhamiaji, Godfey Ngwijo alidai hana kumbukumbu ya makosa ya nyuma kwa washtakiwa, hivyo wahukumiwe kwa mujibu wa sheria.

Washtakiwa katika utetezi wao, waliiomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kuwa wana familia zinazowategemea na waliingia nchini kutafuta chochote kwa sababu Malawi kuna njaa.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa walitenda kosa hilo Januari 25 mwaka huu eneo la Morocco wilayani Kinondoni, Dar es Salaam walikokutwa wameingia na kuishi nchini bila viza halali.



Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro, Dunstan Kyobya (kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Guy Williams (katikati), alipotembelea kujionea uzalishaji sukari na maendeleo ya mradi wa upanuzi wa kampuni hiyo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chongolo aibana wizara mpango utoaji wa dawa

**Na Augusta Njoji,** SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo ameitaka Wizara ya Afya ibainishe mpango wa Bohari ya Dawa (MSD) wa kupeleka dawa na vifaa tiba kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati zilizojengwa nchini ili kutoa huduma kwa wananchi.

Chongolo aliagiza hayo jana wilayani hapa alipotembelea Hospitali ya Wilaya ambayo baadhi ya miundombinu imekamilika lakini vifaa ikiwamo vitanda na vifaa vya maabara havijafika licha ya kuagizwa kutoka MSD.

"Ninakwenda kukaa na Waziri wa Afya aniambie mpango wa MSD kupeleka dawa na vifaa tiba kwenye hospitali na vituo vya afya vilivyojengwa nchini. Majengo yakikamilika yanapaswa kutoa huduma," alisema.

Chongolo pia aliahidi kumfikishia Rais Samia Suluhu Hassan ombi la kuongeza fedha za kumalizia ujenzi wa hospitali hiyo.

Pia alimbana Mwenyekiti wa Halmashauri ya Singida, Elia Diga baada ya kutoa majibu yasiyoridhisha kwa wananchi kuhusu wananchi kulazimishaa kulipa fedha za matibabu kabla ya kupata huduma.

Akiwa kijijini Mntiko, Chongolo alipokea malalamiko hayo, mkazi wa kijiji hicho, Jamal Kyoka akisema wanapokwenda hospitalini, wanatakiwa kulipa fedha kwanza, hali inayowaweka hatarini kufia kwenye benchi wakisubiri kukamilisha mchakato wa malipo.

"Unatakiwa kuwa na fedha ulipe kwanza, anakwenda mjamzito tumeambiwa atatibiwa bure lakini anatozwa Sh. 100,000 hadi 200,000," alilalamika. Kutokana na malalamiko hayo, Katibu Mkuu Chongolo alimtaka mwenyekiti huyo kujibu hoja hizo na kwanini wanatangulia kudai fedha kabla ya huduma.

Akitoa majibu ya malalamiko hayo, mwenyekiti huyo alisema kuna malipo ya papo kwa papo ambayo mtu analipa Sh. 7,000 huku akiendelea kupata huduma na ndicho kinachofanyika.

"Kinachofanyika kwenye hospitali zote za serikali ni hiki labla kwenye Hospitali ya Masista," alisema. Majibu hayo yaligomewa na wananchi na Katibu Mkuu Chongolo kusisitiza wananchi wanatakiwa kupata huduma ndipo walipie.

Alimwagiza mwenyekiti kuhakikisha utaratibu unaotakiwa unafuatwa ipasavyo ili kuondoa malalamiko kwa wananchi ya kulipishwa kabla ya huduma.

# Adaiwa kujinyonga kisa deni la 8,000/-

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

MTOTO Jafari Bakari mwenye umri wa miaka 16, mkazi wa Kijiji cha Mnima, Kata ya Mnima mkoani Mtwara, anadaiwa kujinyonga porini kisa Sh. 8,000 aliyokuwa akidaiwa na rafiki yake.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi Isack Mushi alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea majira ya jioni baada ya Jafari kuondoka nyumbani kwao na kwenda kusikojulikana.

Alisema kwa mujibu wa mashuhuda walioona mwili huo, waliukuta porini ukiwa unaning'inia juu ya mti kwa kutumia kamba ngumu.

Kamanda alisema chanzo cha kifo hicho kimetokana na mwili kukosa hewa ya kutosha baada ya kubanwa na kamba aliyoitumia kujinyonga.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa mtoto huyo alikuwa anadaiwa Sh. 8,000 na rafiki yake ambapo hata hivyo mama wa marehemu alizilipa ili kuondoa usumbufu kati yao.

Alisema kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea ili kubaini sababu za kufanya uamuzi wa kujinyonga.

Dada wa marehemu, Sharifa Bakari alisema kuwa kabla ya mwili huo kukutwa porini, alimwona akipigwa vibaya na kijana ambaye hakumfahamu, hali iliyomsababishia kuingiwa na wasiwasi.

Alisema kuwa baada ya kipigo hicho alimwona mdogo wake akikimbilia maeneo ya porini na alipomfuatilia alikuta akiwa amejinyonga kwa kamba.

"Imeniumiza sana kifo cha mdogo wangu kwa sababu nimeshuhudia kwa macho yangu kabla ya kujinyonga, amepigwa kipigo kibaya, na nikamwona anakwenda porini nilipofuatilia kumbe alipigwa kwa ajili ya deni la Sh. 8,000 na ndipo kaamua kujinyonga," Sharifa alidai.

Selemani Mtunga, mkazi wa kijiji hicho alidai kuwa majira ya saa 12 jioni alimwona mtoto huyo anapigwa maeneo mbalimbali ya mwili na kijana aliyemtaja kwa jina moja la Mkuruduku.

"Alieleza kuwa anamdai (Jafari) Sh. 8,000 na kwamba alipokwenda kununua samaki na alitoa Sh. 2,000 na kutaka samaki ila kwa bahati mbaya, alirudishiwa Sh. 10,000 na hakurudisha hata baada ya kufuatwa," alidai.



# 'Wakuu wa Magereza watapimwa kwa utendaji na si vinginevyo'

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

MKUU wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Ramadhani Nyamka amesema atawapima wakuu wa magereza wote nchini kwa utendaji kazi wao na si vinginevyo.

Kamishna Jenerali Nyamka alitoa kauli hiyo jana wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa mwaka 2022/23 wa Wakuu wa Magereza na maofisa waandamizi wa jeshi hilo uliofanyika jijini hapa.

Alisema lengo la mkutano huo ni kujadili utekelezaji wa majukumu ya msingi kwa maofisa magereza nchini kwa kuwa wao ndio wako na askari, wafungwa na mahabusu.

Kamishna Jenerali alisema maelekezo mengi ameyatoa kwa barua na njia ya simu lakini hilo pekee halitoshi, ndio maana wameandaa mkutano mkuu kwa ajili ya kupeana maelekezo ya kiutendaji.

"Maagizo mengi nimeyatoa kwa njia ya simu na barua lakini hilo pekee halitoshi. Wakati mwingine unatakiwa kukutana na wakuu uso kwa uso ili kuona kitu cha ziada," alisema.

Kamishna Jenerali Nyamka alisema kuwa baada ya kikao hicho, watajua nani atoke na nani abaki kwa sababu tayari watakuwa wamepeana maelekezo ya kutosha ya kiutendaji ambayo wanatakiwa kuyafanya.

Alifafanua zaidi ya kuwa jeshi hilo linataka kuona kuna weledi katika utendaji kazi kwa sababu jamii inataka kuona matokeo chanya ya Jeshi la Magereza katika kazi zao za kila siku ambazo wanafanya.

Kutokana na hilo, kiongozi huyo alisema maagizo ya safari hii atayatoa kwa msisitizo na kuongeza kuwa atakayekiuka, hatua kali zitachuliwa dhidi yake kwa sababu tayari atakuwa ameshapata maelekezo katika mkutano mkuu wa mwaka.

Alisema kuwa mambo yakiwa mabaya wa kunyooshewa kidole ni yeye na hilo hatalikubali na kama mtu asipotimiza wajibu wake, lazima aondolewe kwa sababu sheria inaelekeza kila mmoja anapaswa kuwajibika kwenye kazi ambayo amepangiwa.

Alisema utaratibu wa jeshi kuwa na vikao vya aina mbalimbali unalenga kukumbushana wajibu, majukumu pamoja na kubaini changamoto katika utendaji kazi wa kila siku, hivyo wanapaswa kusikiliza kwa makini mada zitakazojadiliwa ili kuzifanyia kazi.

"Tunataka kubaini changamoto, mafanikio na namna ya kujipanga ili kutekeleza majukumu ya kila siku kwa urahisi," alisema Kamishna Jenerali Nyamka. Naibu Kamishna wa Jeshi la Magereza, Jeremiah Katungu alisema moja ya ajenda ambazo zitajadiliwa katika mkutano huo wa siku mbili ni namna ya utunzaji siri na nyaraka za jeshi.

Naibu Kamishna huyo aliwataka Wakuu wa Magereza pamoja na maofisa waandamizi wa jeshi hilo kuhakikisha wanazingatia mada zitakazojadiliwa kwenye mkutano huo ili wazifanyie kazi kwa ufasaha.




Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Ramadhan Nyamka, akizungumza na maofisa waandamizi wa jeshi hilo, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka 2022/2023 wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya msingi, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## SIDO yanoa wanawake usindikaji wa mazao

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI ya Wanawake na Uchumi wa Viwanda (WAUVI) Mkoa wa Dodoma imepatiwa mafunzo ya ujasiriamali na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kwa udhamini wa serikali ili kukuza ujuzi wa shughuli mbalimbali za usindikaji mazao ikiwamo ubuyu, zabibu, karanga na pilipili.

Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha mazao hayo yaongezewa thamani ili wapate mkopo unaotolewa na serikali kwa wanavikundi mbalimbali wakiwamo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Akizungumza na wanachama wa taasisi hiyo, Rehema Mbeleke ambaye ni Mwenyekiti wa WAUVI Mkoa wa Dodoma, alisema kuwa baada ya kupatiwa mafunzo watahakikisha wanaongeza thamani ya mazao hayo.

"Taasisi hii ya MAUVI baada ya kupatiwa mafunzo na SIDO, watakuza thamani ya mazao hayo ambayo yanapatikana Dodoma kama vile ya zabibu, karanga na ubuyu na hatimaye kupata masoko nchini na nje ya nchi," alisema. Aliwataka wanachama hao kutumia mitandao ya kijamii katika kutangaza biashara zao ili kupata wateja wa bidhaa zao nje ya nchi, huku akiwahiadi taasisi kuwatafutia masoko ya nje.

Mwenyekiti wa WAUVI Wilaya ya Dodoma Mjini, Zabibu Shaibu alisema hadi sasa wametengeneza vikundi 35 ambavyo vitapatiwa mafunzo.

Aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kupatiwa mafunzo ili kujitengenezea kipato ukizingatia kuwa taasisi hiyo inajihusisha na kuwainua kiuchumi wasindikaji wa bidhaa hizo.

# Wanufaika mikopo halmashauri waonywa matumizi kwenye anasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAWAKE walionufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri wameonywa matumizi ya fedha hizo katika anasa badala yake wazielekeze kwenye miradi ya kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Wanawake wa Kanisa la Tanzania Assembles of God (TAG) Jimbo la Dodoma Kati Mnadani Revival Temple Dodoma, Elizabeth Mwayi, alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhi msaada wa sabuni za kufulia kwa wagonjwa waliolazwa wodi ya kinamama na watoto kwenye Hospitali ya Rufaani ya Mkoa wa Dodoma.

Aliyataka makundi ambayo yanayokopeshwa mikopo hiyo na kujishugulisha na ujasirimali, kuwa waaminifu kwa kurudisha kwa wakati ili wengine waweze kukopa.

Alisema mikopo hiyo inayotolewa na halmashauri, ni kwa ajili ya kuyasaidia makundi ya wanawake vijana na watu wenye ulemavu ili wajikwamue kichumi na siyo anasa.

Mwenyekiti huyo pia aliiomba serikali kupitia halmashauri zake kuendelea kutoa elimu ya uelewa kuhusu kuwasaidia watu wenye mahitaji, akisisitiza kuwa jamii ya watanzania inapswa kuwa na moyo wa kujitoa kwa mali na fedha kusaidia wenye uhitaji wakiwamo wagonjwa, yatima, wajane na wenye ulemavu ili wapate mahitaji yao ya kila siku.

Mwenyekiti huyo alisema tabia ya kuwasaidia watu wenye uhitaji ni agizo la Mungu, pia kuisaidia serikali ambayo imekuwa ikiyategemea madhehebu na taasisi za dini kushiriki katika kuwakwamua wasiojiweza kiuchumi.

"Leo tumeambatana na kundi hili la wanawake ikiwa ni siku yetu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake wa Kikristo (WWK), tunaungana pia na serikali kuhakikisha tunaisaidia katika kuwapatia misaada watu wasiojiweza," alisema.

Aliongeza kuwa taasisi na madhehebu ya dini na vikundi vya kinamama na vijana wanatakiwa kuunga mkono juhudi ambazo zimekuwa zikisadia katika kuwakomboa wanyonge na wenye mahitaji maalum ili wamudu maisha yao ya kila siku.

Akizungumza wakati wa kutoa misaada kwa wagonjwa, kiongozi huyo pia aliziomba taasisi na madhehebu ya dini kuendelea kushirikiana na serikali katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiroho ili watu wapate mahitaji yao muhimu.





# Mwinyi awaita Wafilipino uwekezaji sekta ya utalii

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali yake ina mengi ya kujifunza kwa nchi ya Ufilipino iliyofanikiwa katika sekta za mafuta na gesi, utalii, uvuvi na afya.

Aliyasema hayo juzi Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Balozi wa Ufilipino nchini, Marie Charlotte.

Alisema utalii ni sekta mama kwa uchumi wa Zanzibar na kumshauri Balozi Charlotte kuangalia fursa za uwekezaji ili kuitangaza zaidi Zanzibar huko Ufilipino.

Alisema Zanzibar ina idadi ndogo ya raia wa Ufilipino na ushirikiano huo utasaidia kuongeza idadi ya raia wa Ufilipino visiwani humo.

Rais Dk. Mwinyi pia aliwakaribisha raia wa Ufilipino kuwekeza kwenye sekta ya uchumi wa bahari kwa sababu ina mawanda mapana ya uwekezaji na faida kubwa kwa pande zote mbili za ushirikiano.

Balozi Charlotte alisema wataongeza uhusiano wa kidiplomasia uliopo baina ya nchi hizo na ataitangaza Zanzibar kwa kushawishi wawekezaji kutoka nchini kwake kuwekeza kutokana na fursa zinazopatikana kwenye visiwa hivyo.

Balozi huyo pia aliisifu Zanzibar na kusema mazingira yake yanafanana sana na Ufilipino na alishangazwa na utamaduni wa watu wa Zanzibar kwa ukarimu wao kwa wageni, unatofautiana kidogo na ule wa Wafilipino.

Uhusiano wa Diplomasia baina ya Tanzania na Ufilipino ulianza tangu Desemba 15 mwaka 1961 kwa pande mbili hizo kufungua ofisi za kidiplomasia na kushirikiana kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo, jamii na uchumi.




Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na wawekezaji wa Kiwanda cha kuchakata samaki cha Fungurefu, wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Jin-Il Kim (wa nne kushoto), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# 'Maendeleo bora ya familia yanahitaji wanawake mahiri'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman amesema jamii inapaswa ifahamu kwamba maendeleo bora ya familia yanahitaji wanawake mahiri.

Amesema wanawake hao ni wenye uthubutu wa kujenga ushawishi katika kubuni na kutekeleza mikakati na mipango ya maendeleo kwa jamii.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake Migombani mjini Zanzibar alipokutana na timu ya utunzi wa kitabu cha mchango wa wanawake kinachoitwa 'Nyayo za Wanawake Zanzibar', iliyoongozwa na Meneja wa Mradi wa Uandishi wa kitabu hicho, Hannah MacCarriok kutoka Sweeden.

Alisema wanawake ni nguzo muhimu katika kutoa mchango wa kuleta mabadiliko ya maendeleo kwa muda mrefu katika sekta na maeneo mbalimbali.

Makamu wa Rais alisema mchanganyiko wa maisha na utamaduni wa watu kutoka makabila tofauti Zanzibar umesaidia wanawake kutoa mchango wao katika harakati za kupatikana haki na maendeleo. Aliwapongeza washiriki wa utunzi wa kitabu hicho ambacho kimechukua muda wa miaka mitatu kukamilika, akiamini kitasaidia kuionyesha jamii mchango wa wanawake katika maeneo mbalimbali.

Othman aliwataka watunzi hao kuangalia maeneo mengine zaidi ili kupanua wigo katika kukifanyia mapitio na hatua ya utoaji wa toleo la pili la kitabu hicho ili kuongeza mambo mengi zaidi ya mchango wa wanawake yatakayoanishwa kwenye kitabu hicho.

Meneja wa Mradi wa Utunzi na Uandikaji wa kitabu hicho, Hannah MacCarriok alisema mchango wa mabadiliko katika jamii unaweza kufanywa na wanawake kutoka katika ngazi zote ndani ya jamii.

Alisema kitabu hicho mbali na kuonyesha machango wa wanawake, pia kinalenga kuwasahihisha na kuwajengea uwezo na uthubutu wa kushiriki katika masuala muhimu kwa maendeleo yao na taifa.

## Zanzibar yaridhishwa na 'ustaarabu' wa kisiasa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad amesema ameridhishwa na uendeshaji wa mikutano ya hadhara iliyoanza ma kumalizika kwa amani.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake makao makuu ya jeshi hilo mjini Zanzibar wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema mikutano hiyo imefanyika bila matusi, kashfa wala vurugu na hakukuwa na uvunjifu wa amani.

Alisema kuwa kabla ya mikutano hiyo kuanza, Jeshi la Polisi lilikaa pamoja na viongozi wa vyama vya siasa katika kuhakikisha mikutano hiyo inafanyika kwa amani na utulivu.

"Tunashukuru hadi sasa mikutano ya kisiasa inakwenda vizuri, hatujapokea malalamiko ya watu kutukanwa au kuvunjiwa heshima, tunawaomba viongozi wa vyama vya siasa kuendelea na utaratibu huu waliouanza ili kuendeleza amani ya nchi," alisema.


Kiongozi huyo wa polisi alisema mikutano hiyo iliyorejea tena baada ya kuwapo zuio kwa miaka saba, viongozi wa kisiasa wamezingatia muda wa kumaliza wa saa 12 jioni na taratibu nyingine.

"Tunashukuru kuwa viongozi wa vyama vya siasa wametuelewa wameheshimu muda wa kumaliza mikutano yao lakini pia ile mihemko ya kisiasa ya kurushiana maneneo ya kashfa haikuwapo," alisema kamishna huyo.

Alisema jeshi litaendelea kulinda raia na mali zao wakati wote ili kuhakikisha amani inaendelea kutawala muda wote.

Aliwataka maofisa, wakaguzi na askari wa jeshi hilo kuendelea kusimamia kikamilifu jukumu la kuweka ulinzi na usalama na kutokuwa kikwazo kwa mikutano hiyo ya hadhara.

Aliwataka askari kuepuka kutumia nguvu zisizo za lazima endapo kutatokea migongano na badala yake busara na hekima zitumike ili mikutano hiyo iendelee kufanyika bila ya kuvunja sheria za nchi.



RAYVANNY
UKURASA 14



Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# HAIWAHUSU!

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Barnaba amewaambia watu wanaomfuatilia kuhusu kubadili kwake dini na kuwa Muislamu kuwa suala hilo haliwahusu , hivyo wanatakiwa kuacha mara moja.

Akizungumza hivi karibuni, Barnaba ambaye sasa anaitwa Mohamed, amesema kila mtu duniani ana dini ambayo anaifuata na endapo anaona anata kubadili, hilo ni utashi wake binafsi na hakuna sababu ya watu kushangaa na kumuona kama mtu wa ajabu.

Ameongeza kwamba hata kwenye maisha kuna chaguo, unaweza kumuacha rafiki kutokana na kumuona hamjaendana.

"Kila mtu akiniona ananipa hongera, hongera ya nini nimemuoa mke wa mtu? Nataka wanipe hamasa kutokana na kazi zangu nzuri na sio kwa suala la kubadili dini," amesema Barnaba.

Amesema kimsingi yeye anafuata misingi ya maisha aliyojiwekea, kamwe hawezi kusikiliza maneno ya watu kwa sababu hawampatii chochote.

"Nashangaa watu wamelichukulia kama jambo la kushangaza ni maamuzi yangu tu na sio kutokana na shinikizo la mwanamke. Nataka waache jambo hili, maisha yangu nayapanga mimi mwenyewe siangalii watu wanasema vipi," ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Dr Karimu, arudi kivingine



MSANII wa Mziki wa kizazi kipya anayefanya vizuri kwenye gemu,Mboka Mwaijonga, maarufu Dr Karimu, ametangaza kurejea tena jukwaani baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu.

Dr Karimu, ambaye aliwahi kutamba na ngoma kama asali, na salamu salamu na kushirikishwa kwenye albumu ya Madee, amesema kukaa kimya kwenye gemu ni kutokana na matataizo ya kifamilia, pamoja na kuyumba kiuchumi.

Hata hivyo ameamua kuibuka upya kuitetea nafasi yake ambapo hadi leo ameisha tengeneza ngoma mbili Nichumu na Acha, ambazo anatarajia kuziachia ndani ya mwezi huu.

"Ninawaomba radhi mashabiki zangu, kwa kimya kirefu lakini ninatarajia kuachia ngoma zangu mpya mbili ndani ya mwezi huu hivyo wajitokeze kwa wingi kujionea maajabu mapya niliyokuja nayo, ngoma hizo ni audio na baadaye nitaachia video.

## Yamoto wanawake wamuita 'Baby'



WANAMUZIKI wa kike wanaounda kundi la Yamoto Music, wameanza kuwa gumzo baada ya kuachi ngoma mpya ya singeli inayoitwa Baby.

Kuachiwa kwa wimbo huo ni kama Yamoto imerudi upya katika ladha nyingine ambayo inaanza kuwapagawisha mashabiki wa muziki.

Yamoto wamefanya vizuri na ngoma kadhaa kama Wanyooshe, Mume, Sijaona pamoja na nyingine nyingi.



## Willy Paul useja utauweza?

MSANII wa muziki kutoka Kenya, Willy Paul ametangaza kuwa katika maombi kwa ajili ya kazi yake kubwa na bila ya kuwa na mpenzi.

Msanii huyo amesema kuwa anataka kuwa mseja na hivyo kuwataka wanawake kuacha kumpa vishawishi vya mapenzi.

"Nitabaki kubaki mseja ili tukio langu linalokuja lifanikiwe... nachagua kuwa mtakatifu kabisa... wanawake tafadhali nifanyie rahisi mchakato huu. asante kwa kunielewa," Pozee alitoa ombi kwa kina dada.

# The game of love: Usimdharau Usiyemjua

**Na Adam Fungamwango**

KUNA tabia mbaya sana miongoni mwa jamii ya kuwadharau baadhi ya watu kwa sababu ya muonekano wao usioridhisha, maumbile na hata umasikini.

Na mara nyingi huwa kwa watu ambao hawafahamiki vizuri kwa hao wenye tabia hiyo mbaya.

Kuna watu wakimuona mtu ambaye kwa macho anaonekana kama 'kachoka', hana siha nzuri, nguo zake chakavu, au hajionyeshi na kujimwambafai mbele za watu kama yeye ni nani, basi wanakutana na dharau na manyanyaso sana.

Kwanza kabisa nisema tabia hii ni mbaya sana na haifai, na watu wenye tabia hii wanatakiwa kujirekebisha kwa sababu aliyekupa wewe ndiye aliyemnyima huyo.

Halafu pia kuna baadhi ya watu ambao wana uwezo mkubwa sana kuliko hao wanaoheshimiwa kwa muonekano wao, lakini hawana tabia ya kujionyesha na wanabaki kwenye hali yao ya kawaida tu.

Hayo yameshajitokeza sana na ndiyo maana waswahili wana msemo wao maarufu wa 'usimdharau usiyemjua.'

Usimdharau kwa sababu huwezi kujua ni nani, kwani si watu wote wenye tabia ya kujisifia sana, au kuvaa vizuri ili aonekane ni nani.

Filamu ya 'Kijana Tajiri' imebeba ujumbe huu nitaoutoa hapa. Kijana Kelvin anatokea kumpenda msichana mmoja wa jirani aitwaye Loveness.

Kelvin ni kijana aliyepanga jirani ya kina Love siku chache tu zilizopita. Hata hivyo anakutana na upinzani, matusi, manyanyaso na dharau kutoka kwa binti huyo.

"Siwezi kuwa na mwanaume kama wewe, usinichukulie poa, niangalie juu mpaka chini, hii ni taipu yako? Hujioni ilivyo, kwa hiyo umezunguka kote ukaona mimi ni saizi yako? Utanipa nini wewe,




hizo nguo zako tu zimechanika." Hizi ni moja ya kejeli alizokuwa akipambana nazo Kelvin.

"Kwani mimi nina kasaoro gani, au nina tofauti gani na wanaume wengine?" Anauliza.

"Katafute mwanamke mwingine siyo mimi, nataka mwanaume awe ameshapanga plani zake na ana hivyo vitu, kama majumba, magari, siyo wewe kapuku, tena iwe mwanzo na mwisho, sikupendi, sikuhitaji, sina hisia na wewe, koma."

Wakati Love alikuwa anamsakama Kelvin na maneno hayo machafu, shoga yake ambaye alikuwa mrembo kama yeye, Mahula alikuwa akimuonea huruma sana.

Kuna siku alimfuata, akamuomba radhi kwa niaba ya rafiki yake, anamletea na zawadi ya sambusa, lakini alimwambia maneno machache kuwa pale aligomba mwamba, atafute tu mwanamke mwingine kwa sababu atadhalilika zaidi.

Mara kwa mara Mahula alikuwa akimfuata Kelvin na kumpa moyo kuwa kuna siku atapata mwanamke atakayemthamini.

Mwisho ya siku ikaja kubainika kuwa Kelvin alikuwa mtoto wa tajiri. Alifanya mchezo wa kutoka kwao kwenda kupanga chumba uswahilini ili apate mke bora na si bora mke

"Nilikuwa nataka mwananmke ambaye atanipenda mimi na siyo mali zangu. Ndiyo maana nilifanya hivi na kweli imenisaidia nimepata yule anayenipenda. Naye ni Mahula." Akasema Kelvin na kusababisha kilio na kusaga meno kutoka kwa Loveness.

Love hakuwa na upendo kwa Kelvin, baada ya kufahamu kuwa ni tajiri ghafla akataka 'kujibebisha'. Mahula, ambaye hata hakufikiria, kwa sababu ya kuwa karibu tu na Kelvin alimbembeleza, kumtia moyo, na kumpelekea misaada midogo midogo, akachukuliwa na mtoto wa tajiri kwenda kuolewa.



## Rayvanny hana ugomvi na mtu

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Rayvanny amekana kuwa na tatizo na Harmonize, akieleza wao wanaishi kama ndugu wa familia moja.

Amesema anajitahidi kufanya kazi katika njia nzuri bila kujenga migogoro na wasanii wengine.

Rayvanny amegoma kuzungumzia tetesi za kutoka na mwimbaji Feza Kessy ambaye wameshaonekana pamoja mara kadhaa.

## WANAUME TAFUTENI PESA

**Na Adam Fungamwango**

NIMEPITAPITA kwenye mitandao ya kijamii ya wasanii mbalimbali na watu maarufu kusema kweli wanachangamsha sana kiasi kwamba hivi sasa kuna msemo maarufu sana kuwa 'Bongo kufa kwa 'stresi' ni kujitakia tu. Wengine wanasema 'Bongo mchawi bando tu, wala huwezi kuboreka.'

Leo nimeona niwaletee meseji zilizotumwa au kuandikwa na watu maarufu kwenye jukwaa la mitandao ya kijamii ili nawe msomaji uburudike.

**DIAMOND PLATINUMZ**

Akiwa amejiposti kwenye insta video yake akiwa amevaa mavazi yale ambayo aliyatumia kwenye ngoma inayonyanyasa kwa sasa 'Zuwena' na kuwa na muonekano tofauti na alivyozoeleka, msanii maarufu wa muziki wa bongo fleva nchini Diamond Platnumz aliongea maneno haya.

"Madada zangu mnaojifanya mnanipenda, eti mnanifia, yaani nyinyi mnajifanya hajawahi kunipenda mtu yoyote dunia hii kuliko nyinyi. Eti nyinyi mnanipenda kuliko anavyonipenda Latifa, kuliko anavyonipenda Nasibu, mngenikuta kwenye hali hii sasa hivi, mngenipenda? Nawauliza? Mngenikuta kwenye hali hii, mngeongea maneno hayo? Wanaume tafuteni hela ndugu zanguni."

**JACKLINE WOLPER**

Mcheza filamu wa siku nyingi nchini Jacline Wolper, yeye akajiposti kwenye insta video yake akiwa anasikiliza wimbo wa msanii wa bongo fleva Ali Kiba uitwao 'Mahaba'

Akiwa anasikiliza huku akinesanesa kufuatisha midundo ya ngoma hiyo, akaandika "mahaba kuna wasiokula huko."

Bila shaka alikuwa akimaanisha kipande kilichoonekana kumkuna kinachosema "Sina kumbukumbu ile, uchungu wa kulia 'deile', mapenzi yalinifanya nisile"



**LINAH SANGA**

Ni kama Linah Sanga, mmoja wa wasanii bora wa bongo fleva naye aliimuunga mkono Wolper, kwani mawazo yao yalifanana. Kwenye mtandao wake wa instagram yeye aliandika "Nafsi yangu inasema, bora nimpende tu alienizaa." Maneno hayo naye pia ameyatohoa kwenye ngoma hiyo hiyo ya Ali Kiba.

Lakini yeye alikuwa amechukua kile kipande kinachosema, "Siku hizi hakuna mahaba, mapenzi ya mkataba... Nafsi yake inasema, bora nimpende tu aliyenizaa..."

**SHAMSA FORD**

Msanii mwingine wa kike wa filamu nchini, Shamsa Ford, yeye aliandika kwenye intagram yake kitu kama dongo hivi kwenda kwa watu fulani anaowajua.

"Hivi unajua mfitinishaji anakuua huku unajiona? Popote ulipo wewe kaka upupu ukufate uwashwe na nyuki wakung'ate, lipua likuvimbe ,na hilo shepu lako la kihindi libonyee. Ndugu zangu kuweni makini na hawa wadogo mnaokutana nao mjini na kuwakaribisha kwenye maisha yenu ni nyoka balaa, wengi wao huja kwa masilahi na kukukandamiza."

**IDRISS SULTAN**

Huyu jamaa ni mchekeshaji mzuri tu. Yeye akaenda kwenye peji ya instagram ya msanii Billnass ambaye alijipost yupo kwenye Uwanja wa Ndege hauonekani vema kuwa ni wapi, lakini amebeba mtoto mchanga. Sasa Idriss ambaye hupenda sana kumchokoza msanii huyo kwenye posti nyingi, akaandika.

"Unatembea hatua mbili unaanza kuwaza uache suruali ishuke au umuweke mtoto chini. Vaa mkanda wewe ni mzazi."



# Keke,Darius wapata mtoto

MWIGIZAJI Keke Palmer na mpenzi wake Darius Jackson, wamekuwa na furaha baada ya kumpata mtoto wao wa kwanza.

Habari ya wawili hao kumkaribisha mtoto wao, zilitangazwa kwenye mitandao ya kijamii, huku wakishiriki furaha yao na mashabiki wao.

Palmer, ambaye anajulikana kwa uigizaji wake katika filamu kama vile 'Akeelah and the Bee' na 'Hustlers,' aliweka msururu wa picha kwenye Instagram ambazo zilimuonyesha yeye na Jackson wakiwa na mtoto wao mchanga.





## Kuti acha kuropoka

MWANAMUZIKI anayesifika kwa kusema bila kuogopa nini kitamtokea, Seun Kuti, amesema Wanigeria wamempata kiongozi kati ya mafisadi watatu waliokuwa wakigombea kiti cha urais.

Mwimbaji huyo alizozana na msanii mwenzake, Peter Okoye wa kundi la Psquare, kuhusu nani anafaa kuwa rais.

Seun Kuti aliutaja uchaguzi huo kama uchaguzi uliokwama na kwamba Wanigeria mara kwa mara wanaruhusu takwimu za umma kushawishi uchaguzi wao huku wakijua wanajifikiria wao wenyewe.

## Chameleon azidi kuwakera watu


NYOTA wa muziki wa Uganda, Jose Chameleon, amezidisha mjadala katika mitandaon ya kijamii baada ya kuomba radhi mashabiki wake kwa kumbusu kaka yake Weasel wakiwa jukwaani.

Tukio hilo lilifanyika wakati wa Tamasha la Gwanga Mujje lilofanyika jijini Kampala hivi karibuni.

Ndugu hao walikuwa jukwaani wakitumbuiza, wakati Chameleone alipoelekea kwa Weasel na kumbusu mdomoni, kitendo ambacho kililaaniwa vikali.

Licha ya kuomba radhi, mashabiki wake wameendelea kumshutumu msanii huyo na kueleza anaonyesha mfano mbaya katika jamii.





## Wizkid imekuaje unawanyima raha?

MWANAMUZIKI wa Nigeria Wizkid, amewakasirisha mashabiki wake wa Marekani, baada ya kufuta ziara yake ya muziki nchini humo.

Wiki hii Wizkid ameandika kupitia ukurasa wake wa Twitter, akisema Kwa sababu zisizotarajiwa, amefuta ziara yake ya 'More Love, Less Ego Tour' hadi mwishoni mwa 2023.

Tayari baadhi ya mashabiki walianza kununua tiketi kwa ajili ya kuhudhuria shoo hiyo, lakini amewatoa wasiwasi kwa kueleza waliokata tiketi watapewa kipaumbele.

Burudani hiyo ingefanyika katika ukumbi wa Houston's Toyota Cente na kisha kukamilisha ukumbi wa The Kia Forum jijini Los Angeles.

## Bieber aamua kupumzika

MWANAMUZIKI wa Marekani, Justin Bieber ameamua kuvunja ziara zake za muziki 'Justice World Tour Dates' kutokana na tatizo la kiafya.

Mkali huyo wa RnB, Pop na dance Pop, amesema alielemewa alipokuwa akifanya shoo zake Ulaya mwaka uliopita, sasa ameamua kuchukua mapumziko.

Mara kadhaa aliarisha shoo zake kutokana na matatizo hayo, msimu uliopita aliugua ugonjwa wa kupooza uso unaojulikana kama vile Ramsay Syndrome.





## Simanzi yatanda maziko watoto walioungua moto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

VILIO na simanzi vimetawala kwenye Kijiji cha Kitandu Shinga, Wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro wakati wa maziko ya watoto wawili wa familia moja waliofariki dunia Februari 28 mwaka huu baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto wakiwa wamelala.

Watoto hao ni Greyson Kimaro na Bright Kimaro wenye umri chini ya miaka mitano walikuwamo kwenye nyumba hiyo wakati moto ukianza.

Baadhi ya majirani walilalamikikia walichodai uzembe uliofanywa na babu yao

wakati moto huo ulipotokea.

Samweli Mushi alidai: "Babu aliingia ndani kuokoa televisheni pamoja fedha na kuwaacha watoto hao. Jambo la kuwahi fedha na vitu ni uzembe kwa kuwa mwenyewe alisikika akisema alipoingia ndani kuchukua televisheni, alisikika watoto wakilia lakini hakupata wazo la kuwaokoa kutokana na kuchanganyikiwa."

Akihubiri wakati wa maziko hayo, Paroko wa Parokia ya Uru Mawela, Padri Amos Kibona alisema watoto hao wamezikwa kwa heshima zote za kanisa katoliki licha ya kuwa walikuwa hawajabatizwa kwa kuwa walikuwa a umri mdogo.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanawabatiza watoto wanapofikisha umri wa miaka mitano na kuendelea ili wapate mafundisho yanayotolewa na viongozi wa dini wakiwa wadogo.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Rafael Mushi alisema tukio hilo limeacha pigo kwa wazazi na jamii kwa ujumla huku akiwataka wazazi na walezi kuongeza umakini wanapokuwa na watoto.

"Hatujui chanzo cha moto lakini niwaombe wazazi na walezi kuongeza umakini ili kuhakikisha mnawalinda watoto kwa hali na mali," alisema.

# Adaiwa kujinyonga akiacha ujumbe sababu za kifo aulizwe mama yake

**Na Mary Mosha,** MOSHI

GODSON Mbwambo (30), mkazi wa Pasua Matindigani, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, amefariki dunia akidaiwa kujinyonga na kuacha ujumbe ukutani akieleza kuwa sababu ya kifo chake aulizwe mama yake.

Inadaiwa kuwa Alhamisi ya Februari 23 mwaka huu, kijana huyo alijaribu kujiua kwa kujinyonga kwenye nyumba mbovu iliyoko jirani na kwao lakini aliokolewa na wenzake.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Mtaa wa Matindigani, Amosi Chibago alidai kijana huyo alijinyonga baada ya kujifungia kwenye chumba ambacho ukutani paliandikwa "Kifo changu muulizeni mama yangu".

"Kijana huyo alikuwa anaishi nyumbani kwao na mama yake mzazi, wadogo zake pamoja na wapangaji, lakini alijinyonga kwenye chumba ambacho hakuwa anaishi mtu.

"Jumamosi nilipigiwa simu na balozi akinieleza kijana anayeitwa God amejinyonga. Nilikwenda hadi eneo la tukio na nilipochungulia kupitia dirishani, nilimuona yupo katika hali ya umauti, huku ukutani kukiwa na maandishi 'kifo changu muulizeni mama yangu'," alisema.

Akifafanua zaidi, Mwenyekiti huyo alisema kuwa kwa mujibu wa mama mzazi wa kijana, katika kipindi cha nyuma waliwahi kugombana ingawa walishamaliza kasoro zao. Rafiki wa marehemu, Harison Moleli alidai kuwa marehemu alikuwa analalamika juu ya mama yake kumnyima fedha za matumizi, kumnyanyasa pamoja na kutoa fedha kwa ndugu wengine wasio wa familia.

"Kila mara alikuwa akisema mama yake anamnyanyasa, kumtukana, kuwapa ndugu wasio wa baba yake fedha za mirathi ya baba yake, hali ambayo hakuikubali na aliona kuwa mirathi hiyo haistahili kumsaidia mtu mwingine zaidi yao," alidai.

Balozi wa eneo hilo, Albina Mushi alisema kuliwahi kutokea kutokuelewana kati ya marehemu na dada yake, chanzo kikiwa ni mirathi

"Hapo nyuma ilishatokea kijana huyu (marehemu) na dada mtu kupigana na tatizo lilikuwa ni mambo ya mirathi ambapo marehemu alikuwa anauliza 'mbona wengine umeshawaingizia fedha, bado mimi hujaniwekea?' na baadaye dada mtu alimpiga, lakini mama yake alinielezea hilo na nikaahidi ningemtafuta huyo kijana niongee naye, nilikuwa sijaongea naye hadi tukio hili limetokea," alisema. "Kifo hiki kimetusikitisha sana maana kijana yule tulikuwa tunaishi naye hapa mtaani na alikuwa hana shida na mtu.

"Sasa kilichomsibu hadi kuchukua uamuzi ule wa kujiua hatujui licha ya kwamba aliandika ukutani kwamba kifo chake aulizwe mama yake," alisema Diwani wa Pasua, Pastori Minja.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi, Simon Maigwa alisema kuwa Februari 25 mwaka huu, majira ya saa 12, maeneo ya Matindigani, Godson Mkurya (29) alijinyonga kwa kutumia suruali mbili za jinzi alizoziunganisha na mshipi wa bukta alizotumia kujitundika kwenye kenchi kwenye chumba kilichokuwa kikitumika kufugia kuku na kuacha ujumbe ukutani kifo chake aulizwe mama yake.

"Taarifa kutoka kwa mama mzazi wa marehemu, alidai kuwa mwanawe huyo kila mara alikuwa anamwambia atajiua kwa kuwa amechoka kutokana na ugumu wa maisha, pia mama alieleza kuwa mwanawe aliwahi kufungwa kwa kosa la kujeruhi huko Lupa, Chunya mkoani Mbeya na kufungwa miezi sita huko Mbeya na kuhamishiwa Gereza la Songea mjini.

"Alimaliza kifungo Novemba 19 mwaka jana na kurudi Moshi Desemba 2 mwaka jana na tangu atoke gerezani, alionekana amekata tamaa ya maisha.

"Mama wa marehemu anadai alimtafutia mwanawe kibarua cha kuuza mitumba sokoni Maimoria lakini alifanya kwa muda wa miezi miwili akaamua kuacha na alipoulizwa, alidai amekata tamaa ya kuishi ipo siku atajinyonga.

"Mama alimsihi asifanye hivyo lakini siku ya tukio mama alikuwa amekwenda stendi kukata tiketi kufuatilia mirathi ya mume wake, aliporudi nyumbani ndipo alipomwona mwanawe amejinyonga. Mwili umeshazikwa," alisema kamanda huyo.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, wakati wa mkutano wa faragha kwa mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu, jijini Arusha jana. **PICHA: OWM**

# 100 wajitokeza kuchangia damu

**Na Steven William,** MUHEZA

WATU zaidi ya 100 wilayani Muheza mkoani Tanga wameshiriki uchangiaji damu salama kwa hiari kwa lengo la kusaidia wagonjwa ambao wanahitaji kuongezwa damu hospitalini.

Uchangiaji huo ulifanyika jana kwenye Uwanja wa Jitegemee wilayani hapa, mgeni rasmi akiwa Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Frola Kessy. Uchangiaji damu huo uliambatana na uchunguzi wa afya, upimaji macho na kuhamasisha wananchi kujiunga na huduma za bima ya afya.

Akifungua uchangiaji huo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Frola, alisema upimaji wa afya kwa binadamu ni jambo muhimu, akiwaomba wananchi kujenga utamaduni huo. Alisema kwa sasa kumekuwa na magonjwa mengi, hivyo kuna haja ya watu kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara ili wajitambue mapema na kutibiwa. Alisema wananchi wana wajibu wa kujenga utamaduni wa kuchangia damu salama kwa hiari ili kuwasaidia wagonjwa ambao wanaumwa na wanahitaji kuongezewa damu hospitalini, wakiwamo wanaopata ajali, ikizingatia wilaya hiyo iko barabara kuu.

Flora aliwataka wananchi kukata bima ya afya ili wawe na uhakika wa kupata huduma wakati wowote kwa kuwa kuugua hakupigi hodi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Wilaya ya Muheza, Dk. Gerald Kazumba alisema lengo la shughuli hiyo ni kufanya uchunguzi wa afya ulioambatana na uchangiaji damu salama, upimaji macho na kuhamasisha bima ya afya.

Mganga Msaidizi Hospitali ya Wilaya ya Muheza, Dk. Paul Manjechi alisema katika wilaya hiyo wanaendelea na upimaji wa afya na aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye hospitali na vituo vya afya.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Misemo 'utakiona cha mtema kuni', 'ulimi uliponza kichwa', ilipoanzia

**Na Adam Fungamwango**

NIMEPOKEA simu na meseji nyingi sana baada ya makala iliyopita yenye kichwa cha habari 'hadithi za zamani bila sungura hainogi.'

Watu wengi waliowasiliana na mimi, walisema wamekumbuka mengi, wengine wakinikumbusha vitu vingine ambavyo vilisahaulika kuwekwa.

Kwa kukumbushia tu nilieleza kuhusu watoto wa zamani kupigiwa hadithi na babu na bibi zao, au watu wengine waliowazidi umri.

Hadithi hizo zilizoitwa za mapokeo zilizokuwa zikirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi, zililenga kuelimisha.

Nikaeleza lengo lilikuwa ni kuwaburudisha, kufundisha, kudumisha tamaduni, ikiwemo kuwaepusha watu na matatizo yanayoweza kuwakabili kwa kuwatia hofu.

Ndiyo maana likabuniwa jitu la kutisha lililopachiwa jina la zimwi. Lengo ni kuwafanya watoto wawe waoga kwa kile ambacho wazee wanaona watoto hawatakiwi kufanya, ama kwa wakati wa utoto wao, au maisha yote kwa ujumla.

Wengi walinikumbushia hadithi mbalimbali za wanyama na zingine za wafalme na masultani.

Kwa sasa hakuna wasimuliaji hadithi tena wala wasikilizaji. Wazee wamekuwa na mishemishe nyingi, huku watoto nao akili zao kwa sasa zipo zaidi kuangalia katuni za wanyama, au filamu kwenye televisheni.

Tangu miaka na miaka hadi kizazi cha sasa kumekuwa na misemo mbalimbali inayotumika, lakini asili yake ni kwenye hadithi za mapokeo.

Mfano ni ule unaosema 'utakiona cha mtema kuni.' Huu ni msemo maarufu sana. Ukimfanyia mtu ubaya na akataka kulipa kisasi anaweza kukwambia kwa hasira kuwa 'utaona cha mtema kuni.' Yaani ni lazima tu alipize.

Pale nyumbani mtoto akivunja sahani na mama yupo kazini, dada au kaka atamwambia kwa kumtisha, utaona cha mtema kuni mama akirudi. Maana yake ni kwamba atakaporudi mama utachapwa au kupewa adhabu. Shuleni wanafunzi wamewahi namba, halafu wengine wakachelewa, basi waliowahi watawaambia wenzao kuwa kwa sababu wamechelewa, basi watakiona cha mtema kuni, ikiwa na maana. Una kesi mahakamani, kabla ya kusomwa, anakuja asiyekupenda au ambaye yupo upande wa pili wa kesi hiyo, atakwambia "yaani leo, lazima utakiona cha mtema kuni, lazima ufungwe."



Mtema kuni ni nani? Nadhani wengi wao kizazi hadi kizazi wanautumia msemo bila kujua ulitokea wapi. Leo utajua.

Pia upo msemo mwingine maarufu unaosema 'ulimi uliponza kichwa.' Huu unawahusu watu wanaopenda kuongeaongea sana, au kuropoka vitu visivyowahusu, vile vile kufanya umbea. Nao pia si wengi wanaojua msemo huu umeanzia wapi.

Misemo hii yote imetokana na hadhithi moja tu inayoitwa 'kisa cha mtema kuni.'

Mtema kuni ni mtu anayekata kuni. Hadithi hiyo ya mapokeo inasema hapo zamani alitokea mtema kuni ambaye kazi yake kubwa inayompatia kipato yeye na familia yake ni kwenda porini kukata kuni, halafu akirudi mjini anauza kwa watu mbalimbali kwa ajili ya kushughuli mbali mbali za kupikia.

Siku moja akiwa porini kwa shughuli zake hizo, alifika kwenye mti mmoja ambao alipotaka kuukata ukaomba auache, asiukate.

Mtema kuni alishangaa sana kwa sababu haikuwa jambo la kawaida mtu kuongea kama binadamu. Kwanza alishtuka, mshangao ukafuata baadaye. Lakini akatekeleza ombi la kutoukata. Akakata miti mingine na kuni akazipeleka kuuza mjini kama kawaida.

Siku ya pili akiwa tena porini, alipita pale pale kwenye ule mti. Alipopita tu, ulianza kuongeza. Safari hii si kumuomba usikatwe, bali uliongea maneno yafuatayo."Ulimi uliponza kichwa." Mti ukawa unayarudia maneno hayo mara kwa mara mpaka alipopita.

Tukio la mti kuongea, tena siku mbili mfululizo liliendelea kumfanya mtema kuni awaze sana. Hakumwambia mkewe wala mtu yoyote, lakini ni kama vile alikuwa na dukuduku.

Siku ya tatu akiwa kazini kwake, baada ya kukata kuni zake na kuzibeba akirejea mjini, alipita tena pale pale. Mti uliendelea kuongea maneno yale yale ya siku ya pili, "ulimi uliponza kichwa."

Safari hii hakuvumilia tena, alipofika mjini alianza kuwasimulia majirani wa himaya hiyo anayoishi juu ya kuwepo kwa mti unaoongea kwenye pori lilelo kwenye himaya yao.

Na hata siku ya nne alipokwenda hali ikawa vile vile. Mfalme wa himaya hiyo akasikia habari ambazo zimeanza kusambaa juu ya kwenye himaya yake kuwa kuna mti unaoongea kama binadamu.

Akataka kujua chanzo cha habari hii na ni nani mtu wa kwanza kuiwasilisha. Akaletewa taarifa kuwa hakuna mtu yoyote kwenye himaya hiyo ambaye amewahi kuusikia mti huo zaidi ya jamaa mmoja mtema kuni ambaye kuingia porini kwa ajili ya kukata kuni na kuziuza.

Akaamuru aletwe mbele yake. Watumishi wakampeleka mbele ya mfalme. Akaulizwa kama yale yanayosemwa na yeye ndiye chanzo kiasi cha kuvuma kwenye himaya yake ni ya kweli.

Mtema Kuni alikiri kuwa ni kweli kwenye pori ambalo huwa anakwenda kukata kuni, kuna mti ambao unazungumza yeye ameusikia sasa zaidi ya mara nne kwani hupita hapo hapo kila siku anapokwenda na kurejea kwenye kazi zake.

Mfalme anakamwambia yeye, walinzi, watumishi na baadhi ya mawaziri wake wanataka kwenda kuuona mti huo na kuusikia jinsi unavyozungumza. Lakini kama maneno anayosema hayo si ya kweli, ni lazima apate adhabu. Na hiyo si nyingine bali ni kukatwa kichwa.

Mtema Kuni hakuwa na wasiwasi kwa sababu jambo hilo ni la kweli, akakubali. Safari ilianza, lakini walipofika hapo na kuwaonyesha mti ambao unazungumza kama binadamu haikufanya hivyo.

Zaidi ya masaa mawili mti haikuzunguza lolote. Mfalme akakasirika akaamuru waondoke. Hakutaka kumuadhibu Mtema Kuni, akasema na kesho watarudi tena. Waliporudi hali ikawa ni ile ile. Hii ilimtisha sana Mtema Kuni, kwani sasa alionekana muongo, tena mbaya zaidi mbele ya mfalme.

Siku ya tatu walikwenda tena, ule mti haukuzungumza. Mfalme akamwambia Mtema Kuni angeweza kumkata kichwa siku ya kwanza tu, lakini amemuacha ili kutoa muda kama jambo lile ni la kweli au la. Na kwa jinsi ilivyo, akamwambia kuwa ni muongo, amewaongopewa watu wote wa himaya yake, pamoja na yeye mfalme, hivyo hukumu yake ni kukatwa kichwa, tena pale pale porini na maiti yake iachwe hapo hapo.

Amri ikatekelezwa. Mlinzi mmoja akamkata kichwa Mtema Kuni kwa kutumia jambia. Kichwa kinatenganishwa na kiwiliwili. Cha ajabu ni kwamba baada ya tukio hilo, Mti ulianza kuongea hapo hapo. Na maneno yalikuwa ni yale yale."Ulimi uliponza kichwa."

Mfalme na ujumbe wake ulilia sana, kwani ilionekana kumbe Mtema Kuni hakuwa muongo. Hakupaswa kufa. Akachukua maiti ya Mtema Kuni kwenda kumzika kwa heshima kubwa. Hadithi hii ndiyo iliyozaa misemo miwili maarufu. "Utakiona cha mtema kuni', na,"ulimi uliponza kichwa."

**Tuma meseji 0716 350534**



## Waandamana kudai miundombinu ya reli

**ATHENS,** UGIRIKI

IDADI kubwa ya watu nchini Ugiriki wameingia mitaani kuandamana kupinga hali duni ya miundombuni ya reli baada ya ajali mbaya ya treni iliyosababisha vifo vya watu 57.

Ajali hiyo mbaya ya treni ilitokea Jumanne katika mji wa Larissa baada ya treni ya abiria na ile ya mizigo kugongana. Shughuli za uokoaji zinatarajiwa kukamilika mapema.

Maandamano hayo yalianza Alhamisi jioni, wakati maelfu ya watu walipoingia katika mitaa ya Athens na Thesaloniki kupinga hali mbaya ya miundombinu ya reli nchini humo, ambayo inasemekana kuwa si salama na chakavu. **DW**

## Marekani yatangaza dau nono atakaemuona kiongozi ADF

**WASHINGTON,** MAREKANI

Marekani imetangaza kutoa zawadi ya dola milioni tano kwa mtu atakayetoa taarifa itakayosaidia kukamatwa kwa Seka Musa Baluku, ambaye ni kiongozi wa wanamgambo wa kundi la Islamic State ADF linaloendesha harakati zake nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kiongozi huyo wa ADF anayesakwa ni raia wa Uganda ambaye huenda ana umri wa miaka 40 hivi, kulingana na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani.

"Chini ya uongozi wa Seka Musa Baluku, kikundi hicho kinalenga, kuua, kulemaza, kubaka, na kufanya ukatili mwingine wa kingono na kushiriki katika utekaji nyara wa raia, wakiwemo watoto," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema kundi hilo pia linaajiri na kuwatumia watoto wakati wa mashambulizi na kazi ya kulazimishwa katika eneo la Beni mashariki mwa DRC.

Kundi hilo linatuhumiwa kuwaua maelfu ya raia wa DRC na kutekeleza mashambulizi ya mabomu nchini Uganda.

Mwaka 2020 pekee, kundi hilo linasemekana kuwaua zaidi ya raia 849, kulingana na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. **BBC**



# Marekani yakana kusaidia kuilenga Russia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MSEMAJI wa Wizara ya Ulinzi ya Marekani, Jenerali Pat Ryder amekanusha kuwa wanatoa taarifa kwa wanajeshi wa Ukraine ya data kuhusu shabaha zinazowezekana kushambulia ndani ya Russia.

Akijibu swali la mwandishi wa habari kuhusu shambulio la ndege zisizo na rubani la Februari 28, Ryder alisema ameona ripoti za vyombo vya habari kutoka kwa maofisa wa Russia kwamba Marekani inaweza kutoa taarifa za kufanya mashambulizi hayo.

Alisema Marekani haijafikiria na wala haitatoa habari kama hizo.

"Kama tulivyosema hapo awali, tunashauriana mara kwa mara na Waukraine kuhusu matumizi sahihi ya vifaa ambavyo tunawapa. Tunaona kwamba bado wanalenga kulinda nchi yao na mapigano ndani ya Ukraine. Hiyo ndiyo ninaweza kusema," - alisema jenerali huyo.

Wakati huo huo, Marekani inatarajiwa kutangaza mpango mpya wa msaada wa kijeshi kwa Ukraine.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Taifa, John Kirby, alisema msaada huo utakuwa mada ya mazungumzo kati ya Rais wa Marekani Joe Biden, na Kansela Olaf Scholz wa Ujerumani, wakati viongozi hao wawili watakapokutana katika Ikulu ya White House.


Katika hatua nyingine, imeelezwa mkataba wa START utatumika na Russia kama tishio la nyuklia ili kuzorotesha kasi ya kusaidia kijeshi kwa nchi za Magharibi.

Wataalamu katoka taasisi ya stadi za vita (ISW) wameandika katika ripoti yao kwamba Russia inatumia mkataba huo kama tishio kwa nchi zinazoisaidia Ukraine.

Mazungumzo baina ya waziri wa mambo ya kigeni wa Marekani Anthony Blinken, na Waziri wa mambo ya nje wa Russia, Sergei Lavrov, yaliyofanyika katika kikao cha G20 cha mawaziri kilichofanyika nchini India yalikwama. "Hakuna uwezekano kwamba Russia inatumia hofu ya nyuklia na kufutwa kwa ushiriki wake katika mkataba wa START kwa matumaini ya kupunguza usaidizi wa Magharibi kwa Ukraine na kupunguza kasi ya misaada ya kijeshi ," ISW iliandika.

Blinken alimtaka Lavrov kuondoa marufuku iliyowekewa Marekani ya ushiriki katika mkataba wa START na alielezea utayari wa kushirikiana na Russia katika mkakati wa kudhibiti silaha za nyuklia, bila kujali vita vya Ukraine au uhusiano kati ya nchi hizo mbili.

Blinken aliitolea wito Russia kuacha vita nchini Ukraine, kukaa chini katika meza ya mazungumzo na kuitaka imwachilie Mmarekani Paul Whelan aliyefungwa nchini humo. **BBC**



Baadhi ya mifugo ambayo imekosa malisho na maji baada ya ukame kuikumba mikoa ya Kaskazini mwa Kenya. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Kenya yawahamisha wafugaji kutokana na ukame

**NAIROBI,** KENYA

SERIKALI ya Kenya imeanza zoezi la kuwahamisha wafugaji wanaoishi katika jimbo la Marsabit hadi maeneo ambayo maji yanapatikana kwa urahisi.

Hatua hiyo inatazamiwa kuwaokoa wakazi hao ambao wanaendelea kukabiliwa na hali mbaya ya ukame.

Kupitia mamlaka ya kukabiliana na majanga nchini humo (NDMA),serikali iliamua kuwahimisha wafugaji hao kufuatia ombi la wananchi kutoka sehemu zilizoathirika sana na kiangazi cha muda mrefu.

Mratibu wa NDMA katika jimbo hilo, Mustapha Parkolo alisema kwamba,kufikia sasa familia 131, kati ya 323 tayari zimehamishwa.

"Kule Horr kaskazini,kuna familia zilikuwa zimeomba kuhamishwa kwa sababu walikuwa wamepoteza mifugo yao wakati huu wa ukame.Tunatoa wito kwa mashirika kungana nasi kwa sababu kwa wakati huu,fedha zetu zimepungua kutekeleza zoezi hilo. Tunawahitaji ili kuzihamisha familia hizo hadi sehemu za karibu na maji," alisema Parkolo. Ripoti iliyotolewa na mamlaka hiyo imeeleza kwamba,visa vya utapiamlo miongoni mwa Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano vimeongezeka kwa kiwango kikubwa.

Eneo bunge la Horr Kaskazini linaongoza kwa asilimia 30.3 ya viwango vya utapiamlo,likifuatiwa na Moyale lenye asilimia 15 huku Saku ikiwa na asilimia 8.3.

Hali mbaya ya ukame pia imeathiri sekta ya elimu katika jimbo hilo, japo serikali imeahidi kuwasaidia wanafunzi kuendeleza masomo yao. **BBC**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIANA .J. NTEGI** mwenye picha hapo juu Anatangaza kupotelewa na cheti cha Shahada ya Human Resource Management chenye namba 313C2164/T19 kilichotolewa na Chuo cha Nzumbe University Tawi la Mbeya mwaka 2022.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliana na Juliana Ntegi kwa simu namba **0624262459.**
Taarifa ya Polisi **MBE/MBE/RB/64888/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHUKRAN EDWARD PAULO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba:**S0589-0081** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYABIHORE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SIN/SIN/RB/404217/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**REGINA DANIEL MATINA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC873CRX** aina ya **BOXER.** Chassis No. **BX6LWE91475,** Engine No. **MD2B15**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi. **DOD/DOD/RB/328293/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**JUMA MSTAFA JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 697 BXF.** Aina ya **BAJAJ BEAR.** Chassis No. **MD2A25BZ7HWA23286,** Engine **No. AZZWHA43527.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi. **DOM/RB/35293/2022.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP. 117)**

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED I CLEMENCE PAUL KISIGA** do hereby **ABSOLUTELY** and renounce relinquish and abandon the use of name of **CLEMENCE KISINGA** which appeared in PPF.

For the purpose of evidence of such determination, I hereby DECLARE that she shall at all times here in after in all records, deed, documents and other writings and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the name of **CLEMENCE PAUL KISIGA** his name in lieu of and in substitution of former name of **CLEMENCE KISINGA.**

**AND I DO HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address his BY the adopted name of **CLEMENCE PAUL KISIGA.**

**IN WITNESS WHERE** OF I have set my hands at Iringa, and I hereon substitute the old name of **CLEMENCE KISINGA** by new name of **CLEMENCE PAUL KISIGA.**

SIGNED and DELIVERED by the said
CLEMENCE PAUL KISIGA
Who is known to me personally/identified
To me CLEMENCE PAUL KISIGA

............................
DEPONENT



The latter being known to me personally
In my presence this Day of 28 FEBRUARY , 2023
BEFORE ME:
Name R. TELEMKENI
Signature......................
Postal address 439 IRINGA
Qualification

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANK .M. PAULINE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S4590-0078** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia NAKATUNGURU SECONDARY SCHOOL mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/425071/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......26/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: HAMIS ALLY MSASA WA BOMA ROAD**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: FATUMA JUMA MSASA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 03 mwaka 2022

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY**
**AT MWANZA**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO. 23 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE REVOCATUS MALIBWA LYABANDI (The Deceased)**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICTAION FOR LETTER OF ADMINISTRATION**
**BY: HILLARY LYABANDI (Petitioner)**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of the probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit, before of probate/ letters of administration is made to the above-named petition.
Objection to the grant should filed on or before the 6th day of April, 2023 at 9:00am
No will of the named deceased is deposited and open for inspection at the court.
Dated at Mwanza this 21st day of February, 2023.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT MWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Wilaya ya ..............................TANGA**
**Kituo cha..................MJINI TANGA.................Mkoa TANGA**
**Shauri la Ndoa ..................../2023**
**Jina la Mdai.............MARY CHARLES MPONDA**
**Jina la Mdaiwa ........MAMADOU CISS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)
**Kwa..........................MAMADOU CISS............**
**....................................ENGLAND...............**
Kwa kuwa Mdai ameleta..............MADAI YA TALAKA..............................
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe..09..Mwezi..03..Mwaka..2023.. Saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa Shauri hili ni lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu Shauri hili kwaajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa Shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza Shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe ...03...mwezi.. 03...mwaka...2023
....................................
**HAKIMU**
**FAHAMU:**
1. Iwapo unafikiria kuwa Mashahidi wako hawatohudhuria kwa hiari yao wenyewe unaweza kupewa hati ya kuitwa Shaurini katika Mahakama hii yakuwalazimisha mashahidi wote wahudhurie na kupeleka hati yoyote inayohitajiwa mbele ya Mahakama. Unaweza kuiomba Mahakama kwa kulipa ada ipasavyo.
2. Iwapo unalikubali madai haya ili kuepuka kutimilizwa kwa hukumu ambayo huenda ikawa juu yako au juu ya mali yako au yote mawili, Malipo yalipwe kwa mdai au wadai.

Nimepokea nakala hii ya kuitwa shaurini leo tarehe........mwezi........mwaka..........
................................ (Sahihi ya Mdaiwa)\
Nimewasilisha kuitwa shaurini leo tarehe ...........Mwezi..........Mwaka........................
.......................................
( Sahihi ya Mwasilisha Kuitwa Shaurini)

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**

**MATRIMONIAL CAUSE NO. 2 OF 2023**

**DAUD NYABIRUMO NYABIGESO.................. .........PETITIONER**

**VERSUS**
**SATOKO SUGAYA...........................................RESPONDENT .**

**TO;**
**SATOKO SUGAYA**
**MOSHI**

**NOTICE OF MENTION,**

TAKE NOTICE : That the above case has been fixed for MENTION on 17th March , 2023 at 9:00 am before Hon. ERASTO PHILLY. YOU may appear in person or by an advocate or an agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day any documents under which you intend to rely in support on the above mentioned case.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the **Court this 27th FEB , 2023**
**Resident Magistrate**
**MOSHI**
I HEREBY acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this ...day ...of ...2023
**RESPONDENT**



# HADITHI

# MTAKE MSITAKE-21

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa kiburi baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji na kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yanayopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Adel akazima kitufe cha tepu hiyo na kuendelea kuuangalia umati ambao ulionekana kuchangamka, huku wengine wakionekana kupongezana na kufurahia mbinu ambazo Adel na Mary walizifanya kuwaaminisha watu kuwa mmoja kamwagia mwenzake tindikali kwa lengo la kumpumbaza Usonzo lakini pia kumrahisishia kufanya uchunguzi au upelelezi.

"Ndugu wanakijiji, mpango ulikwenda kama tulivyopanga, sasa tukapanga kwenda ofisini kwa Usonzo. Yeye alijua kuwa mimi nimepelekwa pale ili kudanganywa kuwa nitapelekwa Dar kwa matibabu lakini nitaona, lakini lengo ni kwenda kutelekezwa kama ambavyo walipanga na Mary ili watoroke. Lakini alikuwa hajui kuwa Mary alinipeleka ofisini hapo kwa kazi moja tu ya kumpeleleza, huku mwenyewe akijua mimi sioni.

Humo ndani baada ya kuzungumza naye na alituacha kwa muda wa saa nzima. Kwanza Mary alinisaidia kurekodi mazungumzo kama kawaida, lakini mimi nilipiga picha nyaraka zote muhimu alizokuwa amehifadhi ofisini mwake, lakini nilinyofoa baadhi kwa ajili ya ushahidi ambao ninao na tutaupeleka mahakamani kuonyesha kuwa aliingia mikataba feki ya kuhodhi ardhi ya wanakijiji kwa njia ya udanganyifu. Siku ambayo tulikwenda na Mary ofisini mwake mazungumzo yalikuwa kama ifuatavyo. Akabonyeza tena kitufe kuwasikizishia wanakijiji mazungumzo ya siku hiyo Mary alipokwenda na Adel kwenye ofisi za Usonzo kufanya upelelezi bila yeye kujua.

*********************************************

"Karibuni, ila nilikuwa natoka muda huu kwenda kunywa chai, sijui na nyinyi mnahitaji ili tuongozane?"

"Hapana sisi tumeshakunywa." Mary akajibu haraka haraka.

"Basi nitakuacheni hapa kwa muda kidogo, vumilieni tu jisikieni mko nyumbani, wewe Mary umeshapazoea."

"Ni kweli bosi." Mary akajibu.

Mary na Adel walikaa chumbani humo kwa kiasi cha saa nzima bila mwenyeji wao kurejea. Akarejea baada ya saa moja na robo hivi.

"Samahanini sana, nimechelewa sana, unajua tena, unakwenda huko unakutana tena na watu wengine wenye shida zao."




**"Samahanini sana, nimechelewa sana, unajua tena, unakwenda huko unakutana tena na watu wengine wenye shida zao."**

"Hakuna wasiwasi 'faza'." Adel akajibu. Moja kwa moja Mosha Usonzo akaenda kuketi kwenye kiti chake cha ofisi.

Akamtazama Mary na kumkonyeza. Alikuwa na uhuru wa kufanya chochote kwa sababu alijua Adel alikuwa haoni. Na hatoona licha ya kwamba wanajaribu kumtengenezea mazingira ya kwamba ataona tena wakimpeleka Muhimbili.

"Pole sana kijana."

"Anaitwa Adel bwana, kijana ndiyo nini?"

"Oooh, Adel."

"Ahsante sana bwana mwekezaji, nashukuru, na nimeshukuru sana leo kufika kwa mara ya kwanza kwenye ofisi zako, na kukusikia. Unajua mimi tena ndiyo sioni, ila nakusikia."

"Ooh, vizuri sana, nimependa kitu kimoja, wewe ni mtu wa Mungu sana, umeamua kumsamehe mtesi wako. Amekumwagia tindikali, lakini mmekaa mmeyaongea na kuamua kusameheana, hili ni jambo la kushukuru sana, unajua si wote wenye moyo huo."

"Ni kweli bosi wangu kwa sababu vitabu vya Mungu vinasema samehe saba mara sabini. Mimi sina kinyongo, Mary ni rafiki yangu nilifahamiana naye siku chache tu tangu naingia kijiji hiki, lakini kilichotokea naona kama shetani tu alipita kati yetu."

"Sasa kijana ni hivi, mimi ndiyo niliyetoa pesa kwa ajili ya familia yako hapa kijijini, bibi yako na ndugu zako wengine. Leo pia nitakupa kiasi cha shilingi milioni moja kama pole. Mwezi mmoja na nusu hivi ujao tumepanga mimi na Mary kukupeleka Muhimbili kwa ajili ya matibabu zaidi. Kwa mujibu wa madaktari ni kwamba unaweza kuona tena kama utapelekwa kwenye hospitali zenye vipimo vya kisasa. Kwa hiyo utaondoka hapa ukiambatana na mimi pamoja na Mary, sawa?"

"Nitashukuru sana bosi wangu, na ndiyo maana naendelea kuamini kuwa Mary alipitiwa na kitu ambacho si cha kawaida kufanya tukio hili, haikuwa dhamira yake ya dhati. Mimi binafsi kabla ya kufika hapa nimeongea na Mary na nimekubaliana nalo hilo. Nitakwenda kwenye matibabu na naamini naweza kuona tena."

********************************

Kitufe kilizimwa Adel akakohoa halafu akasema. "Hiyo ndiyo kazi nilikyokuwa naifanya na Mary. Na hata aliporejea alikuta tayari sisi tumeshamaliza kazi. Baada ya kuimaliza nikapeleka vielelezo vyote Makao Makuu na wao ndiyo waliotengeneza mpango huu kuwa ifanye kitu kama sherehe ya wewe kuondoka kijiji hapo na ndiyo siku ambayo wao watakuja kumkamata mwekezaji Usanzo na kundi lake. Mary akaenda tena kwake kumwambia siku ya mimi kuondolewa hapo ili na wao watoroke kwenda Arusha. Usonzo akagharamia sherehe yote hii, lakini hakujua nini ambacho kitampata. Alidhani mimi ndiyo kaondoka kupelekwa Muhimbili ili nikatelekezwe, halafu yeye na Mary wakaambizana waniambie mimi kuwa anapelekwa kutibiwa macho." Baadhi ya waliokuwepo hapo waakangua kicheko kutokana na hila na ujanja mkubwa uliotumika.

"Kusema kweli namshukuru sana dada huyu kwa sababu yeye alikuwa huku na huku. Akiwa kwangu tunapanga mipango ya kweli kwa ajili ya kumuangamiza Usonzo, halafu akienda kwa Usonzo anamlaghai, wanapanga mipango ya uongo dhidi yangu. Yeye mwekezaji anajua ni kweli, kumbe anapigwa changa la macho, ndiyo maana leo tumefikia hapa."

Mkasa mzima sasa ulieleweka ni kitu gani kilisababisha Adel akawa kipofu. Kumbe hakuwa kipofu halisi, ni mpango mkakati kwa ajili ya Usonzo. Mpango umefanikiwa, Adel na Mary walikuwa wameua ndege wawili kwa jiwe moja. Kwanza wamemaliza utawala wa Usonzo wa kumiliki wardhi ya wanajiji cha Maweni, kiasi kwamba sasa kila mmoja atarejeshewa ardhi yake, lakini pia umezima azma ya mwekezaji huyo kumtaka kimapenzi Mary kwa nguvu yake ya mamlaka na pesa.

Jaribio alikolilokuwa analifanya la kutaka kumlazimisha Adel kuondoka jijini hapo, au kumteka lisingefanikiwa kamwe kwa sababu hakuwa raia wa kawaida. Alikuwa ni mtu wa usalama aliyeletwa hapo kufanya kazi hiyo. Angeweza kuwamaliza wote kabla hawajafanya chochote. Makao Makuu hawakutaka ajiingize kwenye masuala hayo kabla kazi mama haijafanyika. Hawakutaka Adel ajulikane kuwa si mtu wa kawaida. Chochote ambacho angekifanya kwa walio taka kumteka kwa sababu ya kuonekana kuwa na Mary, kingeweza kuwashtua wanakijiji na wengine, hivyo mpango ukaharibika. Sasa mambo yamekwisha.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# YANGA PRINCESS YAPANIA KUICHAPA FOUNTAIN GATE

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Yanga Princess imejipanga kuvuna pointi tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate Princess utakaochezwa Machi 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Sebastian Nkoma, alisema wachezaji wake wanaendelea vyema kuelekea mchezo huo ambao wanaamini utakuwa na ushindani wakati wote.

Nkoma alisema wachezaji wake wameahidi kupambana ili kuvuna pointi tatu na kujiimarisha kwenye mbio za kuwania ubingwa wa msimu huu.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi yetu, tutahakikisha tunakwenda kubeba pointi tatu za ugenini, tunajua mechi haitakuwa rahisi," alisema Nkoma.

Aliongeza makosa ambayo aliyaona katika michezo iliyopita ya mzunguko wa kwanza ameyafanyia kazi kwa malengo ya kutojirudia katika michezo inayofuata.

Alisema wachezaji waliokuwa majeruhi wanaendelea vizuri na kikosi chake kitaondoka Dar es Salaam keshokutwa kuelekea Dodoma.

"Jumatatu tunatarajia kuanza safari ya kuelekea Dodoma tukiwa na matumaini makubwa ya kushinda, tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuamini. Ligi ya msimu huu ni ngumu zaidi, timu zote zimeimarika, hatuna mechi rahisi," aliongeza kocha huyo.

Simba Queens ya Dar es Salaam na inayonolewa na Mganda, Charles Lukula, ndio vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 kutoka katika mikoa mbalimbali hapa nchini.




Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddaeus Ruwa'ichi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mbio za Pugu Marathon zitakazofanyika Mei 27, mwaka huu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Pugu Marathon Mei 27

**Na Imani Nathaniel**

MASHINDANO ya mbio za Pugu Marathon yamepangwa kufanyika Mei 27, mwaka huu katika eneo la Hija Pugu, Kisarawe mkoani Pwani, imeelezwa.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddeus Ruwa'ichi, alisema maandalizi ya mbio hizo ambazo zitafanyika kila wiki ya mwisho ya kila mwaka yanaendelea vyema.

Ruwa'ichi alisema lengo la mbio hizo ni kuchangisha fedha kwa ajili ya kuendeleza kituo cha Hija kilichopo Pugu ili kusaidia wagonjwa wenye uhitaji mbalimbali ikiwamo kukarabati nyumba aliyowahi kukaa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

"Tumeandaa mbio za Hisani za Pugu Marathon ambazo zitakuwa zikifanyika kila mwaka, lengo ni kuchangisha fedha za kuendeleza kituo, kutoa misaada kwa wagonjwa katika hospitali mbalimbali, kukarabati nyumba aliyowahi kuishi Baba wa Taifa, kudumisha afya na kujenga utamaduni wa kushiriki michezo," alisema Ruwa'ichi.

Katibu wa Kamati ya mbio hizo, Marceline Nkwere, alisema wanawaomba wadau na makampuni kujitokeza kudhamini ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea.

Alisema washindi wa mbio hizo watapata zawadi mbalimbali ambazo zitatangazwa baadaye pamoja na medali.

Alitaja usajili wa washiriki utafanyika kwa njia ya mtandao na ada ya washiriki wa mbio za kilomita 21 na kilometa 10 ni Sh. 30,000 na zilizobakia ni Sh. 20,000.

## Dodoma Jiji FC wakosa penalti

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Dodoma Jiji inaongoza kwa kushindwa kupachika wavuni penalti katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Dodoma Jiji ambayo ipo katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 24, ndiyo timu iliyofanikiwa kupata penalti nyingi mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, imebahatika kupata penalti sita mpaka kufikia raundi ya 24, lakini imekosa tano na kupata moja tu.

Geita Gold na Prisons ndizo zinaonekana kutumia vyema penalti ilizopata kwani kila moja imepata penalti zote na kutumbukiza kwenye kamba wakati nafasi ya tatu inashikiliwa na Singida Big Stars ambayo imefunga penalti tatu kati ya nne walizopata.

Simba na KMC zimebahatika kuzawadiwa penalti tatu mpaka sasa na imefunga zote wakati mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Yanga na Ruvu Shooting, kila moja imepata penalti tatu, lakini kila moja imekosa moja.

## TADA kuchagua Aprili 2 Dodoma

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya singles ya mchezo wa visible yanatarajiwa kufanyika kuanzia Machi 30 hadi Aprili Mosi, mwaka huu jijini, Dodoma.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Visible Tanzania (TADA), Redempta Mwabesa, alisema lengo la mashindano hayo ni kupata Timu ya Taifa itakayokwenda kushiriki michuano mbalimbali ya kimataifa.

Mwabesa alisema mbali na mashindano hayo, chama hicho kinatarajia kitafanya mkutano mkuu ambao utaambana na uchaguzi mkuu ifikapo Aprili 2, mwaka huu.

"Tunajipanga kufanya mkutano wa uchaguzi ambao utatusaidia kupata viongozi imara watakifikisha mbali zaidi chama chetu," alisema Mwabesa.

Kiongozi huyo amewataka wadau wa mchezo huo kujitokeza kukiunga mkono chama kwa kukamilisha programu ya michezo ya vijana kwenye ngazi ya shule.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MODRIC AIPASUA MADRID

REAL Madrid watatafakari kuhusu majaliwa ya muda mrefu ya Luka Modric mwenye umri wa miaka 37 na kiungo wa Ujerumani, Toni Kroos (33), kabla ya kuamua kumsajili nyota wa England na Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. (***Diario AS***)

### BRUNO AINGIA SOKONI

REAL Madrid pia inawania kumsajili kiungo wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 25, Bruno Guimaraes. (***Mundo Deportivo***)

### LIVERPOOL ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wataongoza mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Chelsea na England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24 wakati wa kipindi cha majira ya joto, baada ya kukataa kukubali kusaini mkataba mpya pale Stamford Bridge. (***Mail***)

### CHELSEA, CITY VITANI

CHELSEA imefufua nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, huku Manchester City na Tottenham Hotspur zikimwania mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia ambaye ana kipengele cha kuondoka kwa pauni milioni 97. ***(Times***)

### KEITA ANUKIA MILAN

INTER Milan ina matumaini ya kumsajili, Naby Keita, mwenye umri wa miaka 28 wakati mkaataba wake na Liverpool utakapomalizika. (***Gazzetta dello Sport)***

### AOUAR KUTUA FRANKFURT

KIUNGO wa Lyon, Houssem Aouar, mwenye umri wa miaka 24 anakaribua kutua Eintracht Frankfurt kwa uhamisho huru baada ya kukataa kuhamia Manchester United. (***Sport1***)

### BARCA KUMUUZA RAPHINHA

BARCELONA inaweza kuwauza nyota wake wakubwa ili kutafuta kiasi cha pauni milioni 178, huku winga wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 26 ni miongozi wanaoweza kuuzwa. (***Sun***)

### ROMEO AGEUKA LULU

KLABU ya Manchester United imejiunga na Chelsea pamoja na Arsenal katika mbio za kuwania kiungo wa Southampton mwenye umri wa miaka 19, Romeo Lavia, ambaye ni raia wa Ubelgiji. ***(Mail***)

### SPURS YAMTAKA SCOTT

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumsajili kiungo wa Bristol City, Alex Scott. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye ni raia wa England pia anawaniwa na Crystal Palace pamoja na West Ham. (***Sun***)

### FERGUSON SOKONI RASMI

LEICESTER City na Everton zinamfuatilia kiungo wa Bologna na Timu ya Taifa ya Scotland, Lewis Ferguson mwenye umri wa miaka 23. (***Nicolo Schira)***

### SOLOMON KUTUA FULHAM

KLABU ya Fulham wanataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu winga wa Israel mwenye umri wa miaka 23, Manor Solomon, kutoka Shakhtar Donetsk ambaye yupo hapo kwa mkopo. (***Standard)***

## DONDOO OKA MAGAZETI LAYA




# KANE ATAKIWA KUTUA UNITED

**LONDON,** England

HARRY Kane anapaswa kuondoka Tottenham Hotspur na kujiunga na Manchester United ikiwa anataka kushinda mataji, kwa mujibu wa Gary Neville.

**Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya England, Kane ametumia muda wake akicheza Spurs licha ya kuhusishwa mara kwa mara na kuondoka, haswa mwaka 2021 wakati alionekana kukaribia kutua Manchester City.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 huu umekuwa msimu wake mzuri akiwa amefunga mabao 18 katika michezo 25 ya Ligi Kuu, lakini bado hajashinda taji kubwa akiwa na Spurs, ambao walitolewa na Sheffield United kwenye Kombe la FA hapo Jumatano.

## ●●● Ni kama nahodha huyo wa England anataka kushinda mataji na...

Akizungumza na Sky Sports News, Neville alipendekeza Kane anatakiwa kuangalia kuendelea mwishoni mwa msimu huu na anaamini United ndio sehemu ambayo itamfaa mshambuliaji huyo.

Alisema: "Kane atataka kushinda mataji. Lakini ikiwa Harry anataka kuondoka huu ndio wakati muafaka.

"Yeye ni mchezaji mzuri, na nadhani kama Kane angeweza kuondoka sasa, anafaa atue Manchester, labda United au City, nadhani angechukua fursa hiyo.

"Ni zaidi ya uwezekano wa kuwa mji kwa sababu ya matumizi yao ya Erling Haaland na kile wamefanya naye, lakini Manchester United wanahitaji mchezaji aina yake.

"Chelsea, siwezi kumwona akienda huko. Yeye hatakwenda Arsenal, Manchester United ndio chaguo pekee kwa Kane msimu huu wa joto.

"Bayern Munich wametajwa. Hiyo inaweza kutokea na nadhani Daniel Levy angefurahi zaidi ikiwa angekwenda mbali zaidi, kwa hiyo tunaweza kuona hivyo.

"Lakini nadhani Harry, ikiwa anataka kushinda mataji, itabidi aondoke Tottenham, kwa sababu Tottenham wanapambana na hali hiyo."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,083,8

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: SIJARIDHIKA NA KIWANGO



**MADRID,** Hispania

XAVI hakuridhika kabisa na uchezaji wa Barcelona licha ya ushindi wa bao 1-0 kwenye El Clasico dhidi ya wapinzani wao Real Madrid katika mchezo wao wa kwanza wa nusu fainali ya Copa Del Rey, na bado anaamini wapinzani wao wana nafasi katika mchezo wa pili.

Bao la kijifunga la Eder Militao katika kipindi cha kwanza pale Santiago Bernabeu lilitosha kwa ushindi wa Barca, wakati Madrid walitawala mchezo wa muda mwingine.

Kocha Mkuu wa Barca alifurahishwa na ushindi huo, lakini alionekana kutoridhika na kiwango cha uchezaji cha timu yake kuelekea mchezo wa marudiano utakaopigwa Aprili 5, mwaka huu.

"Tuna faida fulani," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari.

"Tutalazimika kushindana vizuri katika mchezo wa pili pale Camp Nou. Tumetetea vizuri. Kurudi nyumbani, na mashabiki wetu. Lakini bado naona Real Madrid kama ina nafasi kubwa."

"Sijaridhika ... hatukucheza tulivyotakiwa kucheza," alisema.

"Matokeo yake ni mazuri sana. Nimefurahi na ushindi na mchezo ulikuwa ngumu.

"Ushindi ni mkubwa lakini hatukujua jinsi ya kuweka mpira, ilikuwa ngumu kwetu kushinda. "

# *Mtoto wa Ronaldinho asajiliwa Barcelona*



**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imemsajili mtoto wa gwiji Ronaldinho, Joao Mendes ili apate nafasi ya kufanya makubwa kama baba yake hapo Camp Nou.

Mendes mwenye umri wa miaka 18 alisaini mkataba kujiunga na timu ya vijana ya Barcelona hapo juzi.

Mendes amechukuliwa baada ya kipindi cha majaribio, hapo awali alikuwa akicheza katika klabu ndogo za Brazil.

Katika mashindano yote, Ronaldinho alifunga mabao 98 katika michezo 207 kwa Barcelona wakati wa kipindi cha miaka mitano ya kukaa hapo kuanzia mwaka 2003 hadi 2008.

Alitua hapo baada ya kufanya makubwa kule Paris Saint-Germain na timu ya yaifa ya Brazil akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona.

Wakati maelfu walijitokeza kumkaribisha Ronaldinho mwaka 2003, kusajiliwa kwa mwanawe halikuwa jambo kubwa sana, na Mkurugenzi wa Michezo wa Vijana, Joan Soler Ferre, ndiye aliyemtambulisha.

326,057/-



# JAHAZI LA JAMHURI LAZIDI KUZAMA LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Jamhuri FC imepokea kipigo cha nne mfululizo na kujiweka katika nafasi mbaya katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo inaelekea ukingoni.

Jamhuri ilianza mzunguko wa lala salama kwa kusuasua tofauti na matokeo iliyovuna katika hatua ya awali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu mpya wa Jamhuri, Abdul-Mutik Ali 'Kiduu' alisema kitendo cha kupoteza michezo minne mfululizo kimetokana na ligi hiyo kuwa na kasi kubwa kwa sababu inaelekea mwishoni.

Kiduu alisema wamefungwa na timu zenye ubora na ambazo ziko katika nafasi nne za juu katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar kwenye mashindano ya kimataifa.

Aliongeza unapokutana na timu zinazowania ubingwa, mchezo huwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu kila upande unahitaji pointi tatu muhimu na mwenye bahati huondoka na furaha.

"Kikosi ni kilekile, hakuna mabadiliko makubwa yaliyofanyika, bali ni kasi ya ligi katika mzunguko huu wa lala salama ni ya juu, tunaamini michezo inayofuata tutafanya vizuri zaidi," alisema Kiduu.

Aliongeza bado timu hiyo yenye pointi 29 na iko katika nafasi ya tisa haijapoteza mwelekeo wa kufanya vizuri na anaamini watapata matokeo chanya kwenye mechi zinazofuata.

Alisema wachezaji wake wamejipanga kupata alama tafu katila mchezo wa raundi ya 24 watakaocheza dhidi ya Mafunzo Machi 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan.



Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo akitoa mafunzo kwa washiriki wa kozi ya ukocha ngazi ya CAF B Diploma (hawako pichani), inayoendelea katika Kituo cha Michezo cha Mnyanjani kilichoko jijini, Tanga jana. **PICHA: TFF**

## *Simba: Tumeandaa*

INATOKA UK 24

kwa Horoya AC na kufuzu hatua ya robo fainali.

"Waamuzi wa mchezo wetu dhidi ya Vipers wanatoka Ethiopia ambao ni Bamlak Tessa (mwamuzi wa kati) atakayesaidiwa na Samuel Atango na Tadesse Asseesse na wapinzani wao wanatarajia kutua nchini Jumatatu, mgeni rasmi katika mchezo huu, atakuwa ni Naibu Waziri wa Michezo, Sanaa na Utamaduni, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA', ambaye tunatambua kuwa ni mwenzetu, hatupo tayari kumwangusha," alisema Ahmed.

Alisema wanaingia katika mchezo huo wakiwa na kauli mbiu 'Nguvu moja kwa Mkapa hatoki mtu', tiketi tayari zimeanza kuuzwa na tumeweka kiingilio cha chini Sh. 3,000 ili kila mwanasimba aweze kufika uwanjani kuishangilia timu yake," alisema.

Aliongeza kesho watakuwa na sherehe za hamasa kwenye ufukwe za Coco, ambapo kutakuwa na michezo mbalimbali sambamba na uuzwaji wa jezi na tiketi za kushuhudia mechi hiyo.

## Yanga na shangwe, Fei Toto huyo CAS

INATOKA UK 24

"Jumatano kutakuwa na full shangwe, mashabiki wetu njooni tufurahie pamoja," alisema kwa kifupi kiongozi huyo.

Wakili Karume aliliambia gazeti hili jana wanasubiri hukumu ili waanze taratibu za kupelekea shauri lao katika Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS).

Alisema walitegemea kamati hiyo itatafakari upya uamuzi wa awali kwa kuona wamefuata sheria za mkataba na sio za soka inayoongozwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Kimataifa (FIFA).

Alisema sasa wanasubiri kuona sababu zilizopelekea kamati hiyo kutupilia mbali shauri hilo.

"Mara ya kwanza ameshindwa na tukategemea kuomba marejeo ya shauri letu, tulitarajia kamati itafakari upya na kutumia sheria za FIFA kwa mchezaji anapovunja mkataba.

Sheria za FIFA haitakiwi kumlazimisha mchezaji kucheza katika timu au klabu ambayo hana furaha nayo, kwa kumpa adhabu na kulipa fidia iwe amevunja mkataba kinyume na utaratibu," alisema wakili huyo.

Fei Toto ameendelea kuwa nje ya Yanga tangu Desemba mwaka jana alipotangaza kuvunja mkataba wake na klabu hiyo na kutangaza anataka kwenda kutafuta maslahi bora zaidi ambayo mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara hawakuwa tayari kumpatia hadi anafikia uamuzi huo.

Kiungo huyo aliilipa Yanga Sh. milioni 112 kama ilivyoelezwa kwenye kipengele cha mkataba wake, lakini hata TFF iliamua Fei Toto bado ni mchezaji wa Yanga, Mzanzibari huyo hakuwa tayari kurejea kazini.

Ikaenda mbali zaidi, baada ya mama mzazi kusikika katika vyombo vya habari akitaka mtoto wake atendewe haki na kutolazimishwa kurejea Yanga kwa sababu hana furaha ya kuendelea kuitumikia timu hiyo.


# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/03/23 | 20:30 | Southampton FC vs Leicester City | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 04/03/23 | 20:30 | Tenerife CD vs SD Eibar | 2.36 | 2.80 | 3.40 |
| 03. 04/03/23 | 20:45 | FC Volendam vs FC Emmen | 2.60 | 3.35 | 2.60 |
| 04. 04/03/23 | 22:45 | ACF Fiorentina vs AC Milan | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 05. 04/03/23 | 22:45 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 06. 04/03/23 | 23:00 | CD Mirandes vs Real Oviedo | 2.48 | 2.90 | 3.15 |
| 07. 05/03/23 | 14:30 | Spezia Calcio vs Hellas Verona | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 08. 05/03/23 | 15:30 | Hansa Rostock vs Karlsruher SC | 2.70 | 3.30 | 2.50 |
| 09. 05/03/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Espanyol Barcelona | 2.24 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/03/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Everton FC | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 11. 05/03/23 | 19:30 | Liverpool FC vs Manchester United | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 05/03/23 | 19:30 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.43 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 05/03/23 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 14. 05/03/23 | 21:00 | Santa Clara Azores vs Vitoria SC Guimaraes | 2.70 | 3.15 | 2.60 |
| 15. 05/03/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Go Ahead Eagles | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 16. 05/03/23 | 22:45 | AS Roma vs Juventus Turin | 2.37 | 3.05 | 3.10 |
| 17. 05/03/23 | 22:45 | Stade Rennes vs Olympique Marseille | 2.75 | 3.35 | 2.45 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 04/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1945 | Manchester City vs Newcastle | 1.45 | 4.24 | 6.08 |
| 15:30 | 2373 | Cardiff vs Bristol City | 2.18 | 3.19 | 3.14 |
| 15:30 | 4580 | Blackburn vs Sheffield Utd | 3.34 | 3.39 | 2.02 |
| 16:00 | 4769 | Getafe vs Girona | 2.69 | 2.94 | 2.79 |
| 17:00 | 5571 | Monza vs Empoli | 2.05 | 3.10 | 3.59 |
| 17:30 | 1836 | VfL Bochum vs Schalke 04 | 2.30 | 3.29 | 2.85 |
| 17:30 | 3039 | Augsburg vs Werder Bremen | 2.25 | 3.42 | 2.83 |
| 17:30 | 3674 | Union Berlin vs FC Koln | 1.88 | 3.23 | 4.02 |
| 17:30 | 4047 | Monchengladbach vs SC Freiburg | 2.36 | 3.38 | 2.70 |
| 17:30 | 4419 | Mainz vs Hoffenheim | 1.87 | 3.59 | 3.63 |
| 18:00 | 1387 | Ross County vs Motherwell | 2.51 | 3.10 | 2.75 |
| 18:00 | 1428 | Arsenal vs Bournemouth | 1.23 | 5.49 | 10.63 |
| 18:00 | 1635 | Blackpool vs Burnley | 5.52 | 3.75 | 1.56 |
| 18:00 | 2016 | Wigan vs Birmingham | 2.25 | 3.08 | 3.13 |
| 18:00 | 3832 | Livingston vs Hibernian | 2.86 | 3.20 | 2.37 |
| 18:00 | 4241 | Brighton vs West Ham | 1.75 | 3.54 | 4.23 |
| 18:00 | 4319 | Rangers vs Kilmarnock | 1.16 | 6.73 | 13.85 |
| 18:00 | 4668 | Luton Town vs Swansea | 1.97 | 3.34 | 3.53 |
| 18:00 | 4961 | Wolverhampton vs Tottenham | 3.14 | 3.23 | 2.17 |
| 18:00 | 5095 | Aston Villa vs Crystal Palace | 2.01 | 3.20 | 3.59 |
| 18:00 | 5511 | Hearts vs St Johnstone | 1.68 | 3.69 | 4.53 |
| 18:00 | 5839 | Chelsea vs Leeds | 1.58 | 3.87 | 5.09 |
| 18:15 | 5289 | Burgos vs Granada | 3.40 | 2.81 | 2.28 |
| 18:15 | 5822 | Almeria vs Villarreal | 3.19 | 3.49 | 2.13 |
| 19:00 | 2988 | Lens vs Lille | 2.34 | 3.31 | 2.81 |
| 19:30 | 4344 | Rostov vs Lokomotiv Moscow | 2.09 | 3.29 | 3.24 |
| 20:00 | 4586 | Atalanta vs Udinese | 1.60 | 3.88 | 4.81 |
| 20:30 | 2108 | Tenerife vs Eibar | 2.46 | 2.70 | 3.19 |
| 20:30 | 2276 | Stuttgart vs Bayern Munchen | 5.91 | 4.61 | 1.42 |
| 20:30 | 2741 | Mallorca vs Elche | 1.68 | 3.37 | 5.63 |
| 20:30 | 4138 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Katamon | 1.35 | 4.43 | 7.00 |
| 20:30 | 4520 | Southampton vs Leicester | 2.62 | 3.21 | 2.52 |
| 20:30 | 5716 | Huesca vs Levante | 3.48 | 2.99 | 2.14 |
| 20:45 | 4772 | FC Volendam vs Emmen | 2.55 | 3.28 | 2.55 |
| 21:00 | 2025 | Dundee Utd vs Aberdeen | 3.06 | 3.36 | 2.17 |
| 21:00 | 2517 | Paris FC vs Guingamp | 1.99 | 3.24 | 3.58 |
| 21:00 | 3335 | Le Havre vs Laval | 1.65 | 3.38 | 5.29 |
| 21:00 | 3338 | Dijon vs Grenoble Foot | 2.36 | 2.90 | 3.10 |
| 21:00 | 3854 | Portimonense vs Sporting Lisbon | 7.49 | 4.73 | 1.35 |
| 21:00 | 4397 | Annecy FC vs Metz | 3.39 | 3.19 | 2.07 |
| 21:00 | 4565 | Asteras Tripolis vs Atromitos | 2.23 | 2.97 | 3.45 |
| 22:00 | 2973 | Feyenoord vs Groningen | 1.19 | 6.47 | 10.79 |
| 22:30 | 3615 | FC Luzern vs FC Basel | 2.43 | 3.41 | 2.62 |
| 22:45 | 4965 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 2.41 | 3.40 | 2.66 |
| 22:45 | 5420 | Fiorentina vs AC Milan | 2.80 | 3.10 | 2.44 |
| 23:00 | 2730 | Paris St Germain vs Nantes | 1.28 | 5.33 | 8.49 |
| 23:00 | 3033 | Twente vs Heerenveen | 1.52 | 4.12 | 5.29 |
| 23:00 | 4595 | Atletico Madrid vs Sevilla FC | 1.69 | 3.60 | 5.00 |
| 23:00 | 5951 | Mirandes vs Real Oviedo | 2.60 | 2.74 | 2.94 |
| 23:30 | 1668 | GD Chaves vs Porto | 9.07 | 5.32 | 1.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Machi 4, 2023



Kane atakiwa kutua United
UKURASA 21



Mshambuliaji chipukizi wa Simba, Mohamed Mussa (kulia), akifunga bao katika mechi ya hatua ya 16 bora ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC) dhidi ya African Sports ya Tanga iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga na shangwe, Fei Toto huyo CAS

**Na Saada Akida**

WAKATI Wakili Fatma Karume amesema wanasubiria nakala ya hukumu kutoka katika Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuhusiana na shauri la Feisal Salum 'Fei Toto', klabu ya Yanga imewaandalia shangwe mashabiki wake kuelekea mechi dhidi ya AS Real Bamako kutoka Mali.

Yanga itawakaribisha AS Real Bamako katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi kuelekea mchezo huo wa kimataifa yanakwenda vizuri na wanaamini wataendelea kuwafurahisha wanachama na mashabiki wao katika michuano hiyo.

Kamwe alisema wachezaji wao wataendelea kupambana kuhakikisha wanashinda mechi hiyo na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo yanayofanyi-

INAENDELEA UK 23

# SIMBA: TUMEANDAA MPANGO KAZI MPYA

## ●●● Lengo ni kupata mabao mengi na kuimaliza Vipers ili kunusa robo...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi mnono wa mabao 4-0 na kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC), Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amesema ameandaa 'mpango kazi' kwa mastraika wake ili kuwaongeza uwezo wa kupachika magoli kuelekea mechi ya kimataifa dhidi ya Vipers FC kutoka Uganda.

Simba itawakaribisha Vipers katika mchezo wa Kundi D wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Jumanne kuanzia saa 1:00 usiku, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wekundu wa Msimbazi wamekuwa wakitengeneza nafasi nyingi lakini washambuliaji wake wakiongozwa na nahodha, John Bocco, Jean Baleke, Habib Kyombo na Moses Phiri, wanashindwa kuzitumia vyema jambo lililoilazimu benchi la ufundi kufanya mabadiliko ambayo wanaamini yatazaa matunda.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema wachezaji wao walicheza vizuri na waliwaheshimu wapinzani wao bila ya kujali wanacheza ligi ya chini.

Mgunda alisema walicheza kwa tahadhari kubwa kwa malengo ya kutafuta matokeo ya ushindi huku katika mchezo huo wakianza kwa kuwatumia wachezaji ambao hawapati nafasi ya kucheza mara kwa mara hasa kwenye safu ya ushambuliaji.

"Niwapongeze wachezaji kwa kupambana, wachezaji wamefuata kile tulichowapa mazoezini na kuhamishia katika mechi, hatuwezi kusema tuna kikosi kipana huku wachezaji wanaokaa benchi ukiwapa nafasi ya kucheza hawakupi kile unachokitaka, kwa kiwango kilichoonyeshwa na vijana wetu tunaweza kujivunia tunakikosi cha ushindani," alisema Mgunda.

Aliongeza wamefanikiwa kusonga mbele katika mashindano ya FA ambayo yanazidi kuwa magumu na sasa wanaendelea kujiandaa kwa michezo ijayo kwa kufanyia kazi madhaifu waliyoyaona ili kukiongezea nguvu.

"Tunatengeneza nafasi nyingi, tunashindwa kuzitumia, ukiangalia katika mechi zilizopita, tumefanyia kazi mapungufu yetu baada ya kurejea nyumbani tulipomaliza mechi ya kwanza dhidi ya Vipers ya Uganda, tunaendelea na zoezi hilo kwa ajili ya kuwajenga washambuliaji kutumia vyema kila nafasi," alisema Mgunda.

Aliongeza katika mashindano yote wanayoshiriki wanahitaji mabao hasa katika michuano ya kimataifa kwa sababu yanaweza kuwasaidia baada ya timu kulingana pointi.

"Lazima tufanye kazi juu ya hilo, wachezaji wote kwa pamoja tutawaeleza mahitaji yetu na faida za kupata mabao, mwisho tutaenda kwenye uwanja wa mazoezi kutekeleza hilo kwa vitendo.

Kuhusu Mohammed ni mchezaji kijana na nafasi anayocheza niliwahi kucheza hapo zamani, mara kadhaa tukiwa kambini benchi la ufundi tunatumia muda wa kuzungumza naye sana, kwa kumpa imani atapata nafasi ya kucheza, na aitumie fursa nafasi hiyo," alisema kocha huyo.

Alieleza kabla ya mechi dhidi ya African Sports, alitumia kumjenga kisaikolojia na kumwamini huku kwa kumweleza akipata nafasi moja anatakiwa kuitumia vyema jambo ambalo alilifanya katika mechi hiyo.

Wakati huo huo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu yao kiliingia kambini jana ili kuendelea na maandalizi ya kuwakaribisha Vipers.

Ahmed alisema lengo kubwa la Simba ni kuhakikisha wanashinda mchezo huo ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kumalizia kuzibakisha pointi tatu nyingine kutoka

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >